# Nipashe

Jumatatu Julai 6, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580276

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

...dian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

215779502

HAKI YETU PROJECT

UNDER THE SAME SUN




## Viongozi watano mbaroni madai utesaji wananchi

UKURASA 3

# Lissu kurejea nchini mwisho wa mwezi

• **Asema** amejipanga kushiriki vikao vya chama vya kujadili kuelekea Oktoba...*Endelea ukurasa 2*

**COVID-19**

'Usichukulie poa unategemewa'

- **Nawa mikono mara kwa mara kwa sabuni na maji tiririka**
- **Kaa kwa kuachiana nafari hatua 2 au 3**
- **Vaa barakoa**
- **Ukikohoa au kupiga chafya ziba mdomo**




Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo, Seif Sharif Hamad, akichukua fomu za kuomba kuteuliwa kuwa mgombea wa urais Zanzibar kutoka kwa Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu katika ofisi za Vuga mjini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

RIPOTI MAALUM

## Kipato kikwazo wazazi kununulia wanafunzi barakoa

UKURASA 4

## Maalim Seif ajitosa urais Zanzibar

• **Aahidi** kuleta maendeleo siku 100, Hashimu Juma Issa achukua fomu CHADEMA.... *Uk. 2*




Mkuu wa Idara ya Oganaizesheni na Uchaguzi wa CHADEMA Zanzibar, Kado Salmini Mwalimu, akimkabidhi fomu mtia nia wa urais wa Zanzibar, Hashim Juma Issa (kulia) jana.




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** **SIMBA SC, YANGA ZABANWA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Maalim Seif ajitosa urais wa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, amechukua fomu ya kuwania urais wa Zanzibar kupitia chama hicho ikiwa ni mara ya sita kuwania nafasi hiyo tangu mwaka 1995, alipokuwa Chama cha Wananchi (CUF).

Akizungumza jana baada ya kuchukua fomu hiyo majira ya saa 4:00 asubuhi katika ofisi za chama hicho Vuga, alisema endapo atapata ridhaa ya kuwaongoza Wazanzibari ndani ya miaka mitano ataleta maendeleo ya haraka kwa siku 100.

Maalim Seif alikabidhiwa fomu hizo na Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu na kusindikizwa na wafuasi wa chama hicho.

Alisema ameamua kuchukua fomu za urais ili chama chake cha ACT -Wazalaendo wamfikirie kuwa mgombea wa chama hicho na kuahidi kuwa endapo atachaguliwa ataleta maendeleo ya haraka.

Alisema lengo kuu la kujitokeza kuchukua fomu ya kuwania nafasi hiyo ni kuiletea maendeleo Zanzibar ndani ya kipindi kifupi na kuwastaajabisha Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla.

"Endapo chama changu kitanipa ridhaa ya kupeperusha bendera ya urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu 2020 na wananchi watanichagua kuongoza Zanzibar, nitaleta maendeleo ya haraka kwa siku 100 tu," alisema.

Alisema kwa sasa anasubiri chama kifanye kazi yake kwa kuchagua mgombea ambaye atapeperusha bendera ya chama hicho katika uchaguzi mkuu.

"Huu si wakati wa kufanya kampeni ndugu zangu waandishi wa habari hivyo, niache nikasome kilichokuwa humu na kuwaachia kazi yake chama changu kukaa na kumchagua yeyote atakayefaa kupeperusha bendera ya chama hichi," alisema Maalim Seif.

Pia, aliwaomba wanachama ambao wana sifa wajitokeze kuchukua fomu ya kuwania nafasi hiyo ya urais wa Zanzibar na nafasi nyingine za uwakilishi, ubunge na udiwani.

Naye Katibu Mkuu wa chama hicho, Shaibu alisema kwamba tangu uchukuaji fomu uanze katika chama chao Julai mosi, wanafarijika kuona wanachama wengi wamejitokeza kuitikia kwa wingi kuchukua fomu kwa nafasi mbalimbali.

"Leo ni mwendelezo wa uchukuaji fomu ambapo umeitikiwa kwa wingi na wanachama wetu ambao wamejitokeza kuchukua fomu ya kuwania nafasi ya udiwani, uwakilishi, ubunge kwa Zanzibar na Tanzania Bara," alieleza Shaibu.

Pia, alisema ACT –Wazalendo itahakikisha zoezi zima la kuomba nafasi mbalimbali litaendeshwa kwa kuzingatia demokrasia, haki na uwazi na chama watakuwa wakali kwa mtu yeyote atakayejishirikisha katika utoaji wa rushwa.

Maalim Seif akipitishwa kugombea nafasi hiyo atachuana na wagombea wengine wa vyama vingine vya siasa huku mpinzani mkubwa akiwa ni kutoka Chama Cha Mapinduzi.

**HASHIMU JUMA ISSA AJITOSA CHADEMA**

Kwa upande wa Chama cha Demokrasiana Mandeleo (CHADEMA), visiwani Zanzibar, aliyechukua fomu ya kuomba kupeperusha bendera ni Hashimu Juma Issa.

Alichukua fomu hiyo jana kwenye Ofisi ya Makao Mkuu Zanzibar, alikabidhiwa na Mkuu wa Idara ya Oganaizesheni na Uchaguzi wa CHADEMA Zanzibar, Kado Salmini Mwalimu.

Haya hivyo, Hashimu hakuzungumza chochote kabla na baada ya kuchukua fomu hizo kuhusiana na mipango, mikakati na mambo anayotarajia kuifanyia Zanzibar ikiwa chana chake kitamteua kugombea na baadaye kuchaguliwa na Wazanzibari kuwa rais wa nane.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Gofrey Nyaisa, akijibu maswali kwa mmoja wa wananchi waliotembelea banda la wakala huo kwenye Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa yanayoendelea kwenye viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere Dar es Salaam. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Lissu kurejea nchini mwisho wa mwezi

**Na Enock Charles**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, kwa mara nyingine amesisitiza kuwa atarejea nchini licha ya wasiwasi uliopo kwa wanachama wa chama hicho na wananchi wengine kuhusu hatima yake.

Akizungumza kupitia mitandao ya kijamii akiwa ughaibuni jana, alisema atarejea nchini mwishoni mwa mwezi huu, ili kuhudhuria vikao vya Baraza Kuu na Mkutano Mkuu wa chama hicho vilivyopangwa kufanyika mwishoni mwa mwezi huu.

"Kuna hofu kwa baadhi ya wananchi na wanachama wetu kuhusu uwezekano wangu wa kurudi nyumbani, endapo nitapata ridhaa ya chama chetu," alibainisha Lissu na kuongeza:

"Ili kuwatoa hofu wananchi na wana-CHADEMA hofu hiyo ya kupandikizwa, ninachukua fursa hii kuwajulisha kwamba ninatarajia kuwapo nchini Tanzania wakati wa vikao vya Baraza Kuu na Mkutano Mkuu mwishoni mwa mwezi huu."

Lissu ambaye yupo nje ya nchi tangu mwaka 2017 baada ya kupigwa risasi zaidi ya 32 na watu wasiojulikana jijini Dodoma wakati akirejea nyumbani kwake kutokea bungeni, ameshaahidi mara kadhaa kurudi nchini bila mafanikio, jambo ambalo limeibua sintofahamu kuhusu hatima yake.

Hata hivyo, Lissu amekuwa akisisitiza nia yake ya kurejea licha ya kuahirisha mara kadhaa, huku akitoa sababu mbalimbali za kushindwa kurejea kila anapoamua kuahirisha safari.

Hata hivyo, juzi alichukua rasmi fomu ya kuomba kuteuliwa na chama chake kuwania urais kupitia kwa wakala wake.

Kuhusu usalama wake atakaporejea, Lissu alibainisha kuwa suala hilo kwake limekuwa gumu, huku akilitupia lawama Jeshi la Polisi nchini kwa kutokujibu barua yake ya kuomba kupewa ulinzi ambayo iliandikwa na Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, kwenda kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP) pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama Mataifa.

Tangu alipopigwa risasi Jijini Dodoma, Lissu ameshakaa nje ya nchi kwa takribani miaka mitatu, ambapo muda mwingi ameutumia katika matibabu yake ambayo yalianzia katika Hospitali ya Mkoa wa Dodoma na baadaye Nairobi nchini Kenya na kuhitimisha Ubelgiji, ambako ndiko anakoishi mpaka sasa.

Mwaka jana Lissu alivuliwa ubunge wake wa Singida Mashariki kwa sababu mbili alizozitoa Spika wa Bunge, Job Ndugai, kuwa ni utoro wa vikao vya bunge na kutojaza fomu za maadili ya umma ambazo kwa kawaida hujazwa na wabunge wote.

Lissu alifungua kesi katika Mahakama Kuu ya Tanzania kupinga kuvuliwa ubunge wake ingawa alishindwa kesi hiyo kutokana na kilichoelezwa na Jaji Sirilius Matupa kuwa maombi ya Lissu kwa kutengua uamuzi wa Spika Ndugai kungesababisha uvunjanji wa Katiba.

Jaji Matupa alisema Lissu alipaswa kufungua kesi ya kupinga uchaguzi wa ubunge badala ya kupinga uteuzi wa Spika, jambo ambalo lingesababisha jimbo kuwa na wabunge wawili.

Juni 22, mwaka huu, IGP Simon Sirro, alipohojiwa na ITV alisema kuwa wanamsubiri kwa hamu Lissu, kwa ajili ya kumhoji ili kupata ushahidi wa tukio la kushambuliwa kwake.

Mwishoni mwa wiki, Lissu alikuwa mtia nia wa kwanza kati ya 11 kwa kuchukua fomu ya kuomba ridhaa ya CHADEMA kupeperusha bendera ya chama hicho katika uchaguzi wa Oktoba mwaka huu.

Fomu hizo zilichukuliwa na wakala wake, David Jumbe, ambaye alisema wataanza kuzijaza na kuzitembeza mikoani kwa ajili ya kupata wadhamini 100 kutoka kanda 10 za chama.

HABARI KITAIFA

# Viongozi mbaroni tuhuma kutesa wananchi

**Na Godfrey Mushi,** HAI

VIONGOZI watano wa Serikali ya Kijiji cha Isuki kilichopo Kata ya Masama Kati, Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, wamekamatwa kwa tuhuma za kuendesha operesheni za ukatili dhidi ya wanawake ambao huwakamata na kuwacharaza viboko 60, kuwatoza fedha na kupakwa 'washawasha' sehemu za siri.

Kadhalika, serikali ya kijiji hicho imekiri kununua pingu ili kutekeleza amri ya wananchi kutotembea usiku, baada ya saa 2:00.

Kutokana na taarifa hizo za kukamatwa, kufungiwa na kuteswa katika mahabusu ndogo ya kijiji hicho iitwayo Golgotha, Mkuu wa Wilaya hiyo, Lengai Ole Sabaya, amefuta utaratibu wa sungusungu kufanya operesheni ndani ya kijiji hicho.

Pia, ameamuru kukamatwa na kuhojiwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), viongozi hao ambao ni Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hicho Rabikira Makere, mjumbe wa serikali ya kijiji, Tekla Assenga na wenyeviti watatu wa vitongoji wanaolalamikiwa kwa unyanyasaji huo dhidi ya raia.

Akieleza namna alivyokamatwa na kuteswa, mmoja wa waathirika wa ukatili huo, Neema Ng'unda, alidai baada ya kukamatwa majira ya saa 1:15 usiku, alifungwa pingu na kupelekwa katika jengo la Golgotha na kupakwa washawasha baada ya kushindwa kulipa faini ya Sh. 30,000.

"Walinifuata baa (kilabu cha pombe), nikiwa nakunywa mbege nilikuwa na bibi yangu na mama yangu mdogo, wakaniambia huu sio muda wa kunywa pombe mwanamke, wakaniambia sasa hivi ni saa 2:00 wakaninyang'anya simu wakanileta hapa Golgotha."

"Mama yangu mdogo akaambiwa anivue nguo nipakwe khafii (washawasha), nikavuliwa akanipaka washawasha."

"Wakaniambia kama hauna hela, lipa Sh. 30,000, nikamwambia sina, nikaweka simu yangu rehani, wakasema kwamba haina thamani. Mheshimiwa Mwenyekiti, akaniambia kama hauna pesa, weka saini ya kupakwa washawasha.

"Nikamwambia sawa mwenyekiti, akaandika na daftari analo na saini niliweka ya kupakwa washawasha."

Muathirika mwingine wa ukatili huo, Ndumiswae Makere, alisema Februari, mwaka huu, akiwa kwenye baa yake, alikwenda mtu aitwaye mama Tajiri (Tekla), akiwa na mwenyekiti wa kitongoji na doria ya watu wanane, wakawaambia watu wako chini ya ulinzi akiwamo shemeji yake na kumfunga pingu.

"Tulipofika kwenye hiyo ofisi tuliwekwa pingu mimi na mtoto wa dada yangu, ikabidi nimpigie simu shemeji yangu na dada yangu wakaja wote. Wakaniambia aliyekuruhusu uuze pombe ni nani, nikasema ni uongozi wa kijiji, nikafunguliwa pingu."

Alipoulizwa Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Rabikira Makere, kuhusu umiliki wa pingu na sheria kandamizi kutumika kutesa wananchi alisema: "Hili la kutotembea usiku tulipitisha hapa katika mkutano wa kijiji na wananchi waliridhia. Pingu tulinunua Moshi Mjini," alikiri Mwenyekiti huyo.

Onesmo Munuo, akizungumza katika mkutano huo alimwomba Mkuu wa wilaya hiyo na timu yake kuwaelimisha kuhusu matumizi ya pingu.

"Mtuelimishe, hivi kweli pingu zinauzwa kama njugu? Kijiji hiki peke yake ndio kina pingu, jaribuni kutuelimisha juu ya matumizi ya pingu na unyanyasaji," alisema Munuo.

Kwa upande wake Ole Sabaya alisema: "Hakuna mtu yeyote mwenye mamlaka ya kuwashurutisha wananchi walale saa 2:00 usiku, isipokuwa Rais John Magufuli. Ni kinyume cha utaratibu na sheria, na ni ukanyagaji wa katiba ya nchi."

Akizungumza juzi katika mkutano huo wa dharura kusikiliza malalamiko hayo, Ole Sabaya alisema serikali imempeleka Ofisa Mtendaji wa Kijiji, Jared Swai, lakini hapewi ushirikiano.

AAMURU WARUDISHE PESA

Kuhusu fedha zilizokuwa zikitozwa kutokana na ukatili huo, Ole Sabaya ameagiza Mwenyekiti wa kijiji hicho, Makere Tekla (mjumbe) na wenyeviti wa vitongoji vitatu wakamatwe na warudishe fedha zote za wananchi ambazo wamezichukua baada ya kuwatesa.

Vile vile, aliagiza kufunguliwa upya kwa kituo kidogo cha Polisi Losaa, ambacho kilifungwa ili kutoa huduma kwa wananchi wa kijiji hicho na vijiji jirani.

"Kuanzia sasa, nisisikie sungusungu anafanya operesheni yoyote kwenye kijiji hiki, badala yake namuelekeza Ofisa Tawala, amuelekeze mshauri wa Jeshi la akiba (Mgambo)."

## David Silinde atimkia CCM

**Na Elizabeth Zaya**

ALIYEKUWA Mbunge wa Momba mkoani Songwe, David Silinde, jana alikabidhiwa rasmi kadi ya uanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Silinde alikabidhiwa kadi hiyo pamoja na wanachama wengine waliohama kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na kujiunga CCM. Tukio hilo lilifanyika Tunduma mjini mkoani Songwe, katika hafla maalum ya kumkabidhi Silinde na wenzake kadi hizo zilizokabidhiwa na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Huphrey Polepole.

Silinde ni miongoni mwa wabunge ambao walifukuzwa uanachama wa CHADEMA baada ya kugoma kutii agizo la chama lililotolewa na chama hicho la kujitenga kwa siku 14 bila kuingia bungeni kwa ajili ya kuchukua tahadhari ya ugonjwa wa corona.

Mbali na Silinde, wengine waliofukuzwa uanachama ni aliyekuwa Mbunge wa Moshi Vijijini, Antony Komu, Joseph Selasini (Rombo) na Wilfred Lwakatare(Bukoba Mjini), ambao wote walikihama chama hicho baada ya bunge kuvunjwa.

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, akitangaza kuwafukuza uanachama wabunge hao, alisema uamuzi huo ulitokana na kikao cha Kamati Kuu kilichokaa kuwajadili na kubaini kwamba walipoteza sifa ya uanachama baada ya kukaidi agizo la chama na kujitangazia mbele ya vyombo vya habari kwamba hawakukubaliana na itikadi za CHADEMA.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akifurahi jambo wakati akisikiliza maelezo kutoka kwa Ofisa Mkuu wa Wateja Wakubwa na Serikali wa Benki ya NMB, Alfred Shao (kulia), alipotembelea Banda la NMB kwenye Maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yanayofanyika katika viwanja vya JK Nyerere Barabara ya Kilwa mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Maofisa Mipango waula uteuzi wa JPM

**Na Maulid Mmbaga**

MAOFISA Mipango wametawala katika uteuzi uliofanywa na Rais John Magufuli wa Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri nne nchini, mwishoni mwa wiki, juzi na jana.

Kati ya walioteuliwa ni Katibu Tawala mmoja, ikiwa ni mabadiliko katika halmashauri tano nchini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Gerson Msigwa, Maofisa Mipango walioteuliwa ni Dancan Thebas, anayekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Newala mkoani Mtwara.

Kabla ya uteuzi huo alikuwa Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Kongwa, mkoani Dodoma akichukua nafasi ya Mussa Chimae.

Mwingine aliyeteuliwa ni Mwailafu Edwin anayekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Nanyamba, mkoani Mtwara, ambaye kabla ya uteuzi huo alikuwa Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Ikungi mkoani Singida, akichukua nafasi ya Osca Ng'itu.

Hassan Njama, ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mvomero, mkoani Morogoro, ambaye alikuwa Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Mji wa Mtwara, anayechukua nafasi ya Florent Kayombo.

Mwingine katika uteuzi huo ni Kanyala Mahinda, anayekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara mkoani Morogoro, kabla alikuwa Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Mkuranga mkoani Pwani, akichukua nafasi ya Francis Ndulane.

Kadhalika Rais Magufuli amemteua Anastasia Tumba kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, kabla ya uteuzi huo alikuwa Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, amechukua nafasi ya Anna-Claire Shija.

Wengine katika uteuzi huo ni Saad Mutambule anayekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Arusha kabla alikuwa Ofisa Mipango wa Jiji la Mbeya, anachukua nafasi ya Alvera Ndabagoye, atakayepangiwa kazi nyingine, Erica Yegella, ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mtwara, kabla alikuwa Katibu Tawala Msaidizi mkoani Mbeya, anachukua nafasi ya Omari Kipanga.

Aidha, Rais Magufuli amemteua Elias Ngwanidako kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Jiji la Mbeya mkoani Mbeya, kabla ya uteuzi huo alikuwa mweka hazina wa halmashauri hiyo na amechukua nafasi ya James Kasusura, ambaye amestaafu.

Waziri Kombo ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Biharamulo mkoani Kagera, awali alikuwa Ofisa Utumishi Manispaa ya Morogoro na amechukua nafasi ya Wendi Ng'ahala.

Rais Magufuli pia amemteua Albinus Mgonya kuwa Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, mkoani Morogoro, ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Rukwa, anayechukua nafasi ya Mohamed Utaly.

Vile vile, Rais amemteua Mariam Mmbaga, kuwa Katibu Tawala Mkoa wa Simiyu, aliyekuwa Mkurugenzi katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), akichukua nafasi ya Jumanne Sagini.

Wateule wote wataapishwa leo asubuhi Ikulu ya Chamwino mkoani Dodoma.

RIPOTI MAALUM

# Kipato chakwamisha wazazi kununulia wanafunzi barakoa

Na Zuwena Shame, IRAMBA

KIPATO kidogo kimesababisha changamoto kwa wazazi wengi kushindwa kuwanunulia watoto wao barakoa katika Kijiji cha New Kiomboi, Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Mkoa wa Singida.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe wilayani humo katika shule za msingi na sekondari, umebaini kuwa tangu shule zifunguliwe Juni 29, watoto wengi wanahudhuria shuleni bila kuvaa barakoa.

Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imetoa mwongozo unaowataka wanafunzi kuanzia miaka miaka minane na wasio na matatizo ya kiafya kuvaa barakoa wanapokuwa shuleni.

Katika Shule ya Msingi ya Igumo, Kijiji cha New Kiomboi, siku ya kwanza ya kuripoti shule ni mtoto mmoja pekee aliyekuwa amevaa barakoa.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Edward Mlundi, alisema uvaaji barakoa ni changamoto kwa watoto wengi shuleni hapo kutokana na wazazi wengi kuwa na kipato duni. "Wazazi wengi wanaona kumnunulia mtoto barakoa ni gharama na kuona bora kutumia hela hiyo kwa shughuli zingine," alisema.

Mlundi alisema siku ya kwanza shule zilipofunguliwa ni mwanafunzi mmoja pekee aliyevaa barakoa na wenzake walimdhihaki kwa kumcheka.

Hata hivyo, Mwalimu Mlundi alisema aliwaelimisha wanafunzi hao umuhimu wa kuwaambia wazazi wao wawanunulie barakoa.

Alisema siku ya pili mwitikio ulikuwa mzuri na idadi ikafikia wanafunzi watatu.

"Hii changamoto ni kuwa wazazi huku vijijini hawana uwezo wa kumudu kununua barakoa kwa ajili ya kuwakinga watoto wao na janga la corona," alisema. Mwalimu Mlundi.

Kuhusu utaratibu wa kuwa na chakula shuleni baada ya muda wa masomo kuongezwa shuleni, Mlundi alisema kuwa kwa sasa bado utaratibu huo haujawekwa sawa kwa sababu likizo ya corona imeleta athari na chakula kilichokuwapo shuleni kama unga wa mahindi na maharage vimeharibika.

Aliongeza kuwa shule ipo katika mchakato wa kutayarisha chakula kilichokuwa stoo ili kutatua changamoto hiyo kwa kuwa hata wanafunzi wa shule ya awali wameshindwa kupata lishe ya uji.

Lailat Amis (10) mwanafunzi wa shule ya Igumo wilayani humo alisema wamepewa elimu juu ya kujikinga na ugonjwa wa corona kama kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni, kuvaa barakoa, lakini mzazi wake hajamnunulia kwa sababu hana uwezo huo.

Lailat alisema kuwa anatamani na yeye angekuwa na uwezo wa kuvaa barakoa kama wengine kwa kuwa ni njia ya kujikinga na corona.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Luzilukulu, Wilaya ya Iramba, mkoani Singida, wakiwa kwenye viwanja vya shule hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Katika Shule ya Msingi Kigeza TANESCO, ambayo ni shule yenye watoto wenye uhitaji maalumu kama wenye uono hafifu, wenye ualbino na ulemavu wa viungo ni watatu pekee waliokuwa na barakoa shuleni.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Andrea Muna, alisema wazazi walipata taarifa kuhusu wanafunzi kuvaa barakoa, lakini mwamko ni mdogo sana hasa ikizingatiwa kipato cha wengi kuwa duni.

Muna alisema pia wazazi hawaoni umuhimu wa kuwapa watoto barakoa kwa sababu hulka ya kusema kuwa katika maeneo wanayoishi hakuna mgonjwa au hata mtu ambaye amefariki kwa ugonjwa huo.

Alisema, uongozi wa shule umejitahidi kwa kuweka ndoo za maji na sabuni kuzunguka shule na hata kwenye mabweni ya wanafunzi ili kujikinga na ugonjwa huo.

Kuhusu suala la chakula kwa watoto shuleni hapo, alisema wa kutwa wanarudi nyumbani kula na kurudi shule, lakini wenye mahitaji maalumu wanakula shuleni.

Pili Salaganda (15), mwanafunzi wa darasa la saba, alisema elimu juu ya kujikinga na ugonjwa wa corona imetolewa vizuri shuleni, changamoto kwao ni barakoa kutokana na mzazi wake kutomnunulia.

Salaganda alisema kuwa mzazi wake hana uwezo wa kumnunulia barakoa na hivyo anajikinga kwa kunawa mikono na maji tiririka na sabuni kwa kuwa shule yao ina vifaa vya kutosha.

Naye Ezekiel Kikwezi (14), akizungumzia likizo ya corona, alisema alikuwa anamsaidia mzazi wake kufanya kazi za nyumbani na kumkwamisha kimasomo kwa kuwa waliporejea shule walianza kurudi nyuma kimasomo.

Akizungumzia uvaaji barakoa alisema atambeleza mama yake amnunulie ili ajikinge na ugonjwa wa Covid-19.

"Najua umuhimu wa kuvaa barakoa, nitambeleza mama yangu aninunulie barakoa na mimi nijikinge," alisema.

Katika Shule ya Sekondari New Kiomboi, yenye idadi ya wanafunzi 595 hakuna aliyevaa barakoa.

Kuhusu suala hilo la wanafunzi kutovaa barakoa, Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Amadeus Kiduu, alisema changamoto hiyo imetokana na mwitikio hasi kwa wazazi wengi kutowanunulia watatoto wao.

Alisema uongozi wa shule unaendelea kuhamasisha wanafunzi kuwaambia wazazi wao umuhimu wa kuvaa barakoa.

Kuhusu wanafunzi wengi kukaa kwenye darasa moja, alisema changamoto ni uchache wa miundombinu ya madarasa.

Alisema kuna madarasa 11 ambayo hayajitoshelezi kuwatenganisha wanafunzi kwa kanuni ya mita moja kama njia moja wapo ya kujikinga na corona.

Akitoa ufafanuzi wa changamoto za shule za msingi, Ofisa Elimu (msingi), Chacha Kehogo, alisema wazazi wengi kipato chao ni duni na hawana uwezo wa kununua barakoa kwa ajili ya watoto wao hasa za kiuuguzi hivyo wanashauri wazazi wawashonee watoto za vitambaa ili kuwakinga watoto na corona.

Alisema pia ni jitihada kubwa kwa sasa ni kuwakinga watoto kwa maji tiririka na sabuni ili waweze kuendelea na masomo yao.

Kuhusu kuongezeka saa za kujisomea, Kehogo alisema kwa sasa ofisi yake ina mkakati wa kuhamasisha walimu kujitolea kufundisha wanafunzi siku za Jumamosi ili kukimbizana na silabasi za masomo hasa kwa wanafunzi wa darasa la nne na la saba ambao bado wanakabiliwa na mitihani yao ya kitaifa.

Vile vile, suala la kukaa mita moja, Kehogo alisema madarasa ni machache na wameshauri kuwa na zamu mbili za kuingia darasani kwa wanafunzi wa shule za msingi wote isipokuwa shule za awali.

Naye Ofisa Elimu Sekondari, Mwanjala Godfrey, alisema idadi na mahudhurio ya wanafunzi baada ya likizo imekuwa nzuri, lakini kuna changamoto za wanafunzi wachache ambao bado hawajaonekana na wanafuatilia kwa ukaribu wazazi na wanafunzi hao kubaini tatizo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Linno Mwageni, alisema ili kukabiliana na changamoto za kielimu baada ya kufungua shule wilayani hapo ameshauri kufanyika vikao vya wazazi wiki ijayo katika shule kadhaa ili wazazi waweze kujionea mazingira ya watoto wao wakiwa darasani hasa kwa upande wa mrundikano wa wanafunzi darasani.

"Wakati wa likizo ilikuwa vigumu kuwaita wazazi kwenye vikao hivyo tutaitisha vikao wiki ijayo wakati wa masomo ili wazazi waone changamoto za watoto wao," alisema.

Kadhalika, alisema wilaya yake imehamaisha shule nyingi kuwa na mikakati ya kujikinga na corona hasa maji tiririka na sabuni kwa wanafunzi wake ili kuwa salama wawapo shuleni.

# IGP Sirro asisitiza usajili wa kampuni binafsi kwenye mfumo

**Na Mwandishi Wetu**

INSPEKTA Jenerali wa Polisi (IGP), Simon Sirro, ameziagiza kampuni binafsi za ulinzi na wafanyakazi wa kampuni hizo kuhakikisha wamesajiliwa kwenye Mfumo wa Kusimamia Sekta ya Ulinzi Binafsi (PSGP) hadi kufikia Desemba 31, 2020.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufanya kikao na wamiliki na wakurugenzi wa kampuni binafsi za ulinzi nchini wiki iliyopita jijini Dar es Salaam, IGP Sirro alisema mfumo huo wa kusajili kampuni na wafanyakazi wake kwenye kanzi data maalum ndiyo njia ya kipekee ya kudhibiti changamoto katika sekta hiyo hususan askari wasio waaminifu.

Alisema mfumo huo ni mzuri na utaboresha sekta hiyo, lakini alisisitiza kuwa elimu zaidi inahitajika kwa wadau.

"Mfumo ni mzuri, lakini kitu kikubwa ni suala la elimu. Watu wakielimishwa nadhani wanaelewa, wakurugenzi wangu (wa kampuni binafsi za ulinzi) wana elimu kubwa na wamekwenda shule wakipata elimu ya kutosha wataukubali mfumo," alisema Sirro.

"Kwa sababu askari leo anafanya uhalifu kwenye kampuni hii na anakwenda kwenye kampuni nyingine kufanya kazi, sasa bila kuwa na mfumo huu huwezi kumtambua huyu askari kwamba ni mbabaishaji," aliongeza.

Aliwaonya baadhi ya walinzi ambao huingia kwenye sekta hiyo wakiwa na lengo la kupeleleza njia zinazoweza kuwasaidia kufanya uhalifu, na kwamba kupitia mfumo wa PSGP watadhibitiwa.

"Kuna baadhi ya askari hawa wa ulinzi binafsi anaingia kufanya kazi kwa lengo la wizi tu, anapelekwa kule anakuwa chambo kujua kinachofanyika ni kitu gani, lakini kwa kutumia mfumo wa PSGP ndiyo njia ya kipekee ya kuweza kudhibiti hili," alifafanua.

IGP aliwaagiza wadau wa sekta ya ulinzi binafsi kukutana tena, kuhakikisha wanatatua dosari zilizopo ili wote kwa pamoja wakubaliane na mfumo huo.

Jeshi la Polisi liliagiza kampuni zote binafsi za ulinzi pamoja na wafanyakazi wa kampuni hizo kuhakikisha wamesajiliwa kwenye PSGP kabla ya mwaka 2021, kwani baada ya Desemba 2020 ambao hawatakuwa wamesajiliwa kwenye mfumo huo hawataruhusiwa kufanya kazi kwenye sekta hiyo.

PSGP imeasisiwa na vyama vinavyosimamia sekta ya ulinzi binafsi, na kutekelezwa na Kampuni ya Datavision International chini ya usimamizi wa Jeshi la Polisi.

Mfumo huo unatumia teknolojia kuwasajili kwenye kanzi data kampuni pamoja na wafanyakazi wa kampuni binafsi za ulinzi, na unasaidia upatikanaji wa taarifa za wadau hao kwa haraka ikiwa ni pamoja na kufahamu historia ya mlinzi husika, afya, tabia na mambo mengine.

Zaidi ya kampuni 174 na wafanyakazi 14,000 wamesajiliwa kwenye mfumo huo hadi kufikia siku ya kikao hicho na usajili unaendelea katika mikoa yote nchini.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, ambaye ni Mbunge wa Ilala, Mussa Azzan Zungu, akizungumza katika semina ya viongozi wa kata na mashina wa CCM Ilala, mkoani Dar es Salaam jana, ili kuwajengea uwezo kujipanga na uchaguzi mkuu ujao. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kairuki ahamasisha uwekezaji kwenye mkonge

**Na Mwandishi Wetu,**
MWANGA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, Angela Kairuki, amewataka wananchi kutumia fursa ya mikopo inayotolewa na halmashauri za wilaya, kwa ajili ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, kuwekeza katika kilimo cha mkonge, ambao imeonekana kuwa na chachu kubwa ya maendeleo.

Kairuki, alitoa rai hiyo jana, baada ya kutembelea shamba la mkonge la Kisangara, lililoko chini ya Kampuni ya Mohamed Enterprises, Wilaya ya Mwanga, mkoani Kilimanjaro na kupewa taarifa ya upungufu wa mashine kwa ajili ya kuchakata zao hilo.

Waziri Kairuki alisema ni fursa kubwa kwa wananchi kujipatia kipato na wanaweza wakajiunga katika vikundi kama na kupewa mkopo, ambao watauwekeza katika ununuzi wa mashine ya kuchakatia mkonge, ijulikanayo kwa jina maarufu kama 'Corona' na kupiga hatua kimaendeleo.

"Nimeelezwa kuwa, kuna upungufu wa mashine za kuchakata mkonge, hivyo wakati mwingine mkonge upo ila hakuna mashine ya kuchakata, sasa viongozi wa halmashauri na hata mkoa, tuendelee kuwahamasisha wananchi wawekeze katika zao la mkonge, ambako kumeonekana kuwa na fursa nzuri," alisema Kairuki na kuongeza: "Tunaweza pia kutumia fursa ya mikopo ya wanawake, kikundi au vikundi vya ushirika vinaweza kuwekeza katika Corona wananchi wachangamkie fursa hii, ili kumaliza tatizo la upungufu wa mashine hizi." Aliwataka viongozi wa halmashauri, kutoa elimu kwa wananchi na kuelezea fursa zilizopo katika mkonge, ili kupanua wigo wa uwekezaji katika kilimo hicho, kwa kuwa mahitaji ya mkonge bado ni makubwa nchini na hata duniani. "Mahitaji ya mkonge bado ni makubwa, hivyo tuendelee kuhamasisha wananchi na kuwapa elimu ili wale wenye maeneo yanayofaa kwa kilimo hicho, waweze kuwekeza huko, lakini pia tunaendelea kukaribisha wawekezaji wengine, kuingia katika uchakataji wa zao hili, kwa kuwa kwa sasa vipo viwanda zaidi ya 11 vikubwa na vya kati vya kuchakata mkonge, na viwanda vidogo zaidi ya 70 kwa ajili ya uchakataji wa zao hili," alisema.

Awali, akizungumza Meneja wa kituo cha uwekezaji Kanda ya Kaskazini, Daudi Riganda, aliutaka uongozi wa shamba hilo, kuongeza uzalishaji na kuwekeza zaidi katika zao hilo ili kutengeneza faida.

"Bado hatujaridhika na mwekezaji ametumia fursa ya uwekezaji katika kilimo hiki cha mkonge, ikilinganishwa na rasilimali ya ardhi aliyo nayo na hali ya hali ya hewa iliyopo, hivyo ningeshauri, wawekezaji watakaopewa nafasi ya kuwekeza katika kilimo cha mkonge, waongeze uzalishaji na kuwekeza kwa tija zaidi," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Thomas Apson, alisema kwa sasa wanajipanga kutoa elimu na kuhamasisha wananchi, kujiingiza katika kilimo cha mkonge, ili kuboresha maisha yao kwa kutumia fursa zilizopo nchini.

## NEC yatakiwa kuwajengea mazingira makundi maalum

**Na Renatha Msungu,**

**DODOMA**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imetakiwa kuweka mazingira mazuri kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kupiga kura kwa usalama katika uchaguzi mkuu uliopangwa kufanyika Oktoba, mwaka huu.

Kauli hiyo ilitolewa jana na wadau wa haki za binadamu katika kikao mkakati juu ya ushiriki wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika nafasi za uamuzi na uongozi kilichowakutanisha wadau mbalimbali vikiwamo vyombo vya ulinzi na usalama, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Mahakama.

Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Mathew Mwaimu, alisema Tume hiyo ina wajibu wa kuwafanya wananchi kushiriki katika uchaguzi vizuri zaidi kama haki yao ya msingi kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni.

Alisema NEC ihakikishe inawaandaa wananchi kushiriki uchaguzi katika mazingira ya amani na kuzingatia misingi ya afya hasa katika kipindi cha ugonjwa wa corona.

Mkurugenzi wa Kituo cha Amani, Haki na Msaada wa Kisheria (PLAJC), Jaruo Karebe, alisema kikao hicho kimelenga kuweka mazingira wezeshi na kuimarisha ushiriki wa watu hao katika mchakato wa uchaguzi na kuendeleza uhusiano imara wa kikazi kati ya asasi za kiraia, taasisi za serikali na vyama vya siasa kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya uchaguzi.

Naye Ofisa kutoka TAKUKURU, Tulibako Minga, aliwaonya wananchi kutojihusisha na masuala ya rushwa kwenye uchaguzi mkuu kwa kuwa hawataangalia jinsia ya mtu bali watawakamata kwa mujibu wa sheria.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF imarisheni ulinzi Ligi Daraja la Kwanza

**WAKATI** tayari Gwambina FC ya jijini Mwanza inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza kutoka Kundi A imeshakata tiketi ya kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao, kumekuwa na malalamiko mbalimbali yanayoendelea kwenye ligi hiyo ya pili kwa ukubwa hapa nchini.

Gwambina FC inayonolewa na mchezaji wa zamani wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Novatus Fulgence ina pointi 44, ambazo haziwezi kufikiwa na timu nyingine katika kundi hilo msimu huu.

Kwa upande wa Kundi B, ambalo Dodoma FC na Ihefu FC ya jijini Mbeya, ambazo zinalingana pointi, zinaendelea kuchuana na kupambana kusaka tiketi ya kupanda daraja moja kwa moja kutoka kwenye kundi hilo.

Kwa mujibu wa msimamo, Dodoma FC inaizidi mabao ya kufunga Ihefu, hivyo umakini na usimamizi unatakiwa kuongezwa katika mechi zinazohusisha timu hizo ili upangaji wa matokeo usitokee.

Nipashe inalikumbusha Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kuhakikisha waangalizi wa mechi za timu hizo na nyingine kuongezeka kwa ajili ya kupata timu zitakazopanda daraja kihalali na si kwa njia za 'ujanjaunjanja'.

Hii inamaanisha kuwa, timu iliyojiandaa vema na iliyopata pointi zake bila ya 'kubebwa', ndio itakayopanda kwa haki, na kwa kifupi itakuwa tayari kukabiliana na ushindani na changamoto mpya kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao wa 2020/21.

Tunasema hivi, kwa sababu tumeshuhudia baadhi ya timu zikipata pointi za mezani kutokana na wapinzani wao kuanzisha vurugu ambazo zimesababisha mechi kuvunjika na hivyo, kamati husika kuamua ushindi mezani.

Baadhi ya mechi huko mikoani zimeonekana zinachezwa katika mazingira yasiyokuwa salama kabla ya kuanza na ikidaiwa yameachwa kwa ajili ya 'kuwabeba' wenyeji katika kampeni 'chafu' ya kuondoka na ushindi.

TFF wakati umefika wa kuhakikisha mechi zote zinachekwa na kumalizika kwa Fair Play, ili mwisho wa msimu bingwa au timu zinazostahili kupanda daraja zifanikiwe na si kuzipa nafasi klabu zisizojiandaa. Tunaamini wachezaji wanaotoka katika timu zinazoshiriki Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Daraja la Pili au mashindano ya Kombe la FA, huungana na nyota waliotamba kwenye Ligi Kuu Bara na wanaocheza soka ta kulipwa kuunda kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars).


Kama malalamiko yameendelea kutolewa katika mechi zinazohusisha vigogo wa soka nchini, Simba, Yanga na Azam, haishangazi michezo mingine ambayo haionyeshwi mubashara hali ni mbaya zaidi.

Tufike wakati, TFF iweke wasimamizi ambao wataandika ripoti zisizokuwa na upendeleo wa upande wowote, kwa malengo ya kusaidia maendeleo ya soka hapa nchini na kutojihusisha na 'kampeni chafu' za kuandaa bingwa au klabu za kupanda daraja.

Kwa kufahamu Tanzania imefuzu kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa wachezaji wa Ndani (CHAN), TFF inatakiwa kumwandalia mazingira rafiki Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Mrundi Etienne Ndayiragije, ili wachezaji atakaowateuwa wawe ni wenye uzoefu, na si wale ambao timu zao zilipata ushindi ambao hauna mashaka. Safari ya Tanzania na klabu zake kufanya vema katika mashindano ya kimataifa, inatokana na wachezaji wake kuandaliwa vizuri kuanzia wanaposhiriki ligi za ndani na wasifikiri nyota hao wanaweza kuimarika wanapokuwa kwenye kikosi cha Stars au pale wanaposajiliwa na klabu kubwa.

Inawezekana kupata bingwa wa uwanjani endapo kila timu itafanya maandalizi yanayostahili kabla ya kuanza msimu na kuachana na mbinu 'chafu' za kutafuta pointi nje ya uwanja.

Nipashe tunakumbusha kuwa, hakuna Ligi Kuu Tanzania Bara imara kama Ligi Daraja la Kwanza na Ligi Daraja la Pili, itachezwa kwa mtindo wa bora liende.




## Muungwana Lazima Nilonge



# Waamuzi wabovu nchini wanakimbiza wadhamini

Na Adam Fungamwango

**TAYARI** Shirikisho la Soka Nchini (TFF), limetangaza kuwafungia waamuzi watatu waliochezesha mechi ya Ligi Kuu Bara, kati ya Yanga dhidi ya Azam FC, iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam Juni 21, mwaka huu, timu hizo zikitoka sare ya bila kufungana.

Taarifa iliyotolewa kwenye ukurasa rasmi wa mtandao ya kijamii wa TFF ni kwamba mwamuzi wa kati, Elly Sasii pamoja na wasaidizi wake, Sudi Lila na Mbaraka Haule wamefungiwa kuchezesha soka kwa muda wa miezi mitatu kwa kutoumudu mchezo huo.

Siku chache baadaye baada ya mechi hiyo, mwamuzi mwingine, Shomari Lawi, aliingia kwenye midomo ya mashabiki wa soka, pamoja na vyombo vya habari, baada ya kutomudu mchezo wa robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA, kati ya Yanga dhidi ya Kagera Sugar.

Kwenye mechi hiyo pia kulikuwa na 'madudu' mengi ambayo yalionekana, mwamuzi huyo kutoka Kigoma, akawa ndiyo gumzo kubwa kuliko mechi yenyewe.

Kwanza kabisa nitoe pongezi kwa TFF na Bodi ya Ligi kwa kutoa adhabu hiyo kwa waamuzi wanaovurunda.

Lakini hapa sijajua kama adhabu hii ni kwa sababu tu Azam iliandika barua, au hata kama isingeandika, waamuzi hao wangeadhibiwa?

Bado mpaka sasa hatujajua hatima ya Lawi na wenzake. Na kingine ninachojiuliza ni kwamba miezi mitatu waliofungiwa kina Sasii inajumlishwa na ile ambayo ligi itakuwa imemalizika?

Nasema hivyo kwa sababu zimebaki mechi chache tu msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara umalizike, na inawezekana kukaa mwezi mmoja au miwili hivi bila ya kuwa na ligi, kabla ya kuanza msimu mwingine.

TFF na Bodi ya Ligi bado hawajafafanua kama miezi ambayo haina ligi inahesabika au la. Kama inahesabika sawa, lakini kama haihesabiki ina maana inawezekana waamuzi hao wakamaliza adhabu zao na kukaa wiki kadhaa tu kabla ya adhabu yao kumalizika. Hapa sidhani kama adhabu hii itakuwa ni adhabu au mapumziko ya kawaida.

Kwa siku za karibuni, waamuzi tena wameshaanza kurejea kwenye hali ile ambayo ilisababisha malalamiko sana kwenye Ligi Kuu Bara.

Nakumbuka baadhi ya utetezi wao ulikuwa kutolipwa stahiki zao, lakini hivi karibuni TFF iliwalipa malimbikizo yao yote na kila mmoja akadhani kuwa watakuwa makini kwa sababu awali walikuwa na msongo wa mawazo.

Haiko hivyo. Wapo baadhi ya waamuzi ambao wameendelea kuchezesha vema na kupongezwa kwa kazi nzuri. Lakini baadhi yao mambo yamekuwa ni yale yale, wakiwamo Sasi, Lawi na wengine wanaopangwa katika mechi zisizotumia macho 'mengi'.

Tukisema ni makosa ya kibinadamu ni sawa, lakini cha kujiuliza ni kwa nini makosa yao yanakuwa yakizipendelea timu kubwa tu? Tukisema hawajui nayo pia si kweli. Hawa hawa kuchezesha mechi nyingi na kuwa makini, lakini sasa cha kushangaza wachezeshe mechi za wakubwa.

Hapa kuna tatizo ambalo TFF na Bodi wanatakiwa kukaa na kuliangalia kwa makini.

Vinginevyo miaka nenda rudi tutakuwa tukilalamika kuwa soka la Tanzania ni la timu mbili tu, Simba na Yanga.

Mashabiki watakuwa wakilalamika kuwa Ligi Kuu haina ushindani.

Lakini ukiangalia kwa jicho la tatu ni kwamba Ligi Kuu Tanzania Bara na hata michuano mingine kama Kombe la FA kwa miaka ya hivi karibuni imekuwa na ushindani mkubwa, lakini tatizo baadhi ya waamuzi wameonekana hawataki soka lijicheze lenyewe na aliyekuwa amejipanga sawa na mwenye uwezo siku hiyo ashinde mechi.

Baadhi ya waamuzi wameonekana kama kukariri kuwa ni lazima timu fulani zishinde hata kama hazina uwezo.

Hii ndiyo inaleta tatizo. Hii inasababisha soka la Tanzania haliaminiki. Wenzetu Kenya na Uganda wameshatoka huko. Sisi inaonekana bado baadhi ya waamuzi wetu wanaamini ni lazima Simba na Yanga washinde mechi hata kama siku hiyo hawakuwa na uwezo au wamezidiwa mbinu.

Hawataki wakifungwe ili wakakae chini na kutafakari wapi wamekosea ili wajirekebishe kuelekea mechi zinazofuata.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

# Waziri apiga stop mgodi kuuzwa

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WAZIRI wa madini Dotto Biteko, amesikitishwa na kitendo cha uongozi wa mgodi wa madini ya almasi Mwadui (Wiliamson Diamond), uliopo wilayani Kishapu mkoani Shinyanga kutaka kuuzwa kienyeji bila serikali kupewa taarifa.

Alibainisha hayo jana alipofanya ziara kwenye mgodi huo, baada ya kuona matangazo kwenye mitandao kuwa mgodi huo unataka kuuzwa, lakini mbia wake ambaye ni serikali hana taarifa hizo.

Alisema kitendo cha mgodi huo wa madini ya almasi kutaka kuuzwa kienyeji, ni kukiuka sheria za nchi, na madini, ambapo walipaswa kwanza kutoa taarifa serikalini ambao ndio wabia wao, ndipo taratibu zingine zifuatwe.

"Serikali kupitia Wizara ya Madini tumesikitishwa sana na kitendo cha kuona kwenye mitandao, kuwa mgodi huu unauzwa bila ya sisi kutokuwa na taarifa zozote ambao ndio wabia wenu kwa asilimia 25," alisema Biteko.

"Hivyo naagiza hadi kufikia Julai 10 mwezi huu, tupatiwa taarifa zote za sababu za kutaka kuuzwa kwa mgodi huu, mbali na hapo tutawachukulia hatua kali za kisheria," aliongeza. Pia alisema sababu ambazo wanazitoa mgodi huo za kusitisha shughuli za uzalishaji na kutaka kuuza, kutokana na kushuka kwa bei ya almasi duniani sababu ya corona haina mashiko, bali wawe wakweli kama wamefilisika.

Kwa upande wake meneja mkuu wa mgodi huo, Ayoub Mwenda, alikiri hawakutoa taarifa serikalini juu ya kutaka kuuzwa kwa mgodi huo, huku wakiahidi kufuata maelekezo yote ambayo yametolewa na Waziri wa Madini.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa, aliipongeza serikali kwa kuisimamia vizuri sekta ya madini, kwa kuondoa migogoro pamoja na kupigania rasilimali za Watanzania na kuinua uchumi wa nchi.

# Lukuvi awaita wenye hati ardhi za miaka 33

**Na Munir Shemweta,**
MUSOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amewataka wamiliki wa ardhi ambao hati zao za ardhi zinaishia miaka 33 kwenda ofisi za ardhi za mikoa zilizoanzishwa hivi karibuni kuzihuisha ili kupatiwa za miaka 99.

Lukuvi alitoa maelekezo hayo Jumamosi mkoani Mara wakati akizindua ofisi ya ardhi Mkoa wa Mara ambayo ni ofisi ya 12 kuzinduliwa ikiwa ni mfululizo wa kuzindua ofisi za ardhi kwenye mikoa mbalimbali nchini.

Alisema kuna baadhi ya wamiliki wa ardhi kwenye mikoa ambao viwanja vyao vimepimwa na michoro kuidhinishwa, lakini hati zao ni za miaka 33 na wamiliki hao watakapoenda kuzichukua wanatakiwa kuziangalia ili zibadilishwe na kupatiwa hati za miaka 99.

"Hati nyingi za wale wamiliki ambao hawajazichukua zimekwisha muda wake, muende kwenye ofisi za ardhi za mikoa, huko mtaelekezwa na wasajili wasaidizi wa ardhi katika ofisi hizo namna ya kuzibadilisha ili mpatiwe za miaka 99," alisema Lukuvi. Kwa mujibu wa Lukuvi, zaidi ya wamiliki wa ardhi 50,000 kwenye mkoa Mara hawajachukua hati za ardhi, wengi muda wa hati zao unaishia miaka 33 na kutaka kufika ofisi za ardhi mkoa wa Mara kurekebishiwa na kupatiwa za miaka 99 ili iwe rahisi kupata mikopo mikubwa.

Akizungumzia uzinduzi wa ofisi ya ardhi mkoa wa Mara, Lukuvi alisema mkoa huo umekuwa na migogoro mingi ya ardhi na kubainisha kuwa uzinduzi wa ofisi hiyo utawawezesha wananchi wa Mara kumaliza migogoro kupitia ofisi hiyo badala ya kuipeleka migogoro kwake.

Aliongeza kuwa, pamoja na wizara yake hapo awali kushughulikia kero na migogoro ya ardhi, lakini tatizo la kimfumo lilikuwa kubwa na kuweka wazi kuwa uzinduzi wa ofisi za mikoa unakomesha kero ambapo sasa hakutakiwa na gharama yoyote kwa mmiliki wa ardhi zaidi ya ile atakayolipia wakati wa kuomba hati.

"Mgogoro wa kimfumo ulikuwa mkubwa zaidi, na leo hii tumekomesha kero na hakuna gharama yoyote mmiliki wa ardhi ataingia kufuatilia hati zaidi ya ile aliyolipa wakati wa kuomba hati, serikali ya awamu ya tano imeondoa kero zote kwa wananchi kwenye utawala wa ardhi," alisema Lukuvi.

Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima, alisema ofisi yake imekuwa ikipokea malalamiko na kero nyingi na kati ya malalamiko 12 anayopokea kwa siku sita yanahusiana na ardhi.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kulia), akipewa maelezo kuhusu huduma na bidhaa za Benki ya NBC na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Theobald Sabi (katikati), alipotembelea banda hilo wakati wa ufunguzi rasmi wa Maonyesho ya 44 ya Kimataifa ya Biashara jijini Dar es Salaam juzi. Kulia kwa Sabi ni Mkurugenzi wa Biashara wa NBC, Elvis Ndunguru. **MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yatambua mchango wa NMB

**Na Mwandishi Wetu**

MAENDELEO makubwa yaliyopatikana nchini katika kipindi cha kwanza cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano yamechangiwa kwa namna mbalimbali na kwa kiasi kikubwa na mchango wa Benki ya NMB, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa amesema.

Alisema hali huyo imetokana na uzalendo wa viongozi wake chini ya Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Ruth Zaipuna, ambaye Waziri Mkuu alisema ni kati ya wakurugezi wanne Watanzania waliyoidia sana Serikali ya Rais John Magufuli kuwahudumia vizuri na kuwaletea maendeleo Watanzania wakati wa miaka mitano ya kwanza ya uongozi wake.

Majaliwa aliyasema hayo na kutoa pongezi hizo alipotembelea banda la Benki ya NMB inayoshiriki Maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) yaliyoanza wiki hii.

"NMB ni benki yetu, na mkurugenzi wake ni mmoja wa wakurugenzi sita walioichangia sana serikali hii, wanne ni Watanzania... Kamwambieni MD wenu, nampongeza sana kwa kazi nzuri sana na kubwa anayoifanya," alisema.

Pongezi hizo alizitoa baada ya kumsikiliza Ofisa Mkuu wa Wateja Wakubwa na Serikali wa NMB, Alfred Shao, katika hotuba yake fupi ya kumkaribisha kiongozi huyo na kumpa maelezo mafupi ya mchango wa benki hiyo katika ujenzi wa taifa na maendeleo ya nchi.

Shao alisema wakati wa Serikali ya Awamu ya Tano, NMB imekuwa mstari wa mbele kuhakikisha ajenda ya uogozi wa Rais Magufuli ya kujenga uchumi wa viwanda kwa ajili ya kulifanya taifa liwe ni nchi ya uchumi wa kati inafanikiwa.

Tayari hilo limefanyika baada ya hivi majuzi Benki ya Dunia kuiweka na kuitangaza Tanzania kuwa mojawapo ya nchi zilizoko kwenye kundi la mataifa yaliyo na uchumi huo endelevu wa kati ambao ni muhimu kimaendeleo na kuwakwamua watu kutoka kwenye lindi la umaskini.

Kwa mujibu wa Shao, mambo yaliyofanywa na Benki ya NMB kupitia uwekezaji kwenye maeneo mengi ya kimaendeleo kwa miaka minne mpaka sasa hivi ni mengi mno.

Hii ni pamoja na mikopo kwa sekta binafsi yenye thamani ya Sh. trilioni 2 ambayo pia imesaidia kwa kiasi kikubwa kuchangia ujenzi wa uchumi wa viwanda. Benki hiyo imetoa Sh. 800 bilioni kusaidia kilimo na mnyororo wa thamani katika sekta hiyo.

Shao alisema mazao yaliyonufaika sana na mchango huo wa fedha kutoka NMB ni pamba, mihogo, alizeti, kahawa na korosho.

"Benki ya NMB imeisaidia pia serikali kupitia kuchangia utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati, zaidi ya Sh. 1.2 trilioni imeishatolewa kusaidia miradi mikubwa ya serikali kama umeme, miradi ya maji, reli ya kisasa (SGR)," alisema.

Majaliwa pia alitoa pongezi maalumu kwa NMB kutokana na jinsi benki hiyo inavyopambana kuboresha maisha ya Watanzania hasa wale wa vipato vya chini wanaoishi vijijini.

## Bosi TAKUKURU ajitosa mgogoro North Mara

**Na Ambrose Wantaigwa, TARIME**

MKURUGENZI wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Brigedia Jenerali John Mbungo, ameagiza kuitwa mara moja wasimamizi wa mgodi wa North Mara na kuhojiwa na taasisi hiyo kutokana na madai ya kuchelewesha malipo ya wafanyakazi wa kampuni hiyo walioumia kazini.

Hatua hiyo ilifikiwa baada ya wawakilishi wa waliokuwa wafanyakazi hao wanaokadiriwa kuwa 44 ambao wanadai kupata ulemavu wa kudumu wakiwa kazini mgodini hapo kufika katika ofisi ya Mkurugenzi wa TAKUKURU mjini Dodoma wakilalamikia kupunjwa malipo yao.

Brigedia Jenerali Mbungo aliliambia Nipashe kwa njia ya simu kwamba wasimamizi wa mgodi huo wanapaswa kujieleza kwa nini wameshindwa kutekeleza malipo halali ya waliokuwa wafanyakazi kwa mujibu wa mikataba yao na kampuni hiyo kwa zaidi ya miaka 10.

"Nilipokea malalamiko kutoka kwa waliokuwa wafanyakazi wa kampuni hiyo iliyopo wilayani Tarime kuhusu kupunjwa malipo yao halali na taasisi yetu (TAKUKURU) imelazimika kumuita meneja wa mgodi huo ajieleze kwanza kwa nini suala la fidia ya kuumia kazini limechukua muda mrefu kutatuliwa," alisema.

Alisema taasisi hiyo ilianzisha uchunguzi kuhusu matukio ya rushwa na matumizi mabaya ya madaraka kuhusiana na malipo ya fidia mbalimbali zinazotekelezwa na mgodi huo kwa wananchi ambao pia wanatuhumiwa kuvamia maeneo yaliyofanyiwa tathmini na kujenga majengo upya kwa ajili ya kudai malipo.

Katika hatua nyingine, aliwaasa viongozi wa serikali ngazi za mkoa na wilaya kutimiza wajibu wao wa kuhudumia wananchi kwa kutatua kero zao kwa wakati maeneo yao kote nchini wakitanguliza uzalendo badala ya kuwaacha wananchi kukimbilia ofisi za kitaifa.

"Matukio ya hivi karibuni kwa wananchi kuamua kukimbilia ofisi kuu za kitaifa na kusubiri kujieleza mbele ya ziara za viongozi wa kitaifa ili kutafuta ufumbuzi wa kero zao, ni ishara kwamba huenda ngazi za chini za utawala zinashindwa kutekeleza wajibu wake ipasavyo," alisema.

Alisema iwapo uchunguzi na mahojiano ya awali pande zote vitaonyesha ukiukwaji wa sheria za kuzuia na kupambana na rushwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wale wote waliohusika kuzuia stahiki halali za wananchi.

Kwa mujibu wa mmoja wa waliokuwa wafanyakazi hao, Raphael Achiando, mgodi huo uliwasimamisha kazi baada ya kuumia kazini na wengi wao kupata ulemavu wa kudumu na hatua za ulipaji wa mafao ya kuumia kazini hazikufuatwa.

# CHADEMA yalia na Ma-DED, wasimamizi wa uchaguzi

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimesema kuwa haikubaliki na haistahili kwa wakurugenzi na wasimamizi wa uchaguzi, kuchakachua matokeo na kumtangaza mshindi ambaye hajashinda.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari, iliyotolewa na Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano CHADEMA, Tumaini Makene, kauli hiyo ilitolewa na Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika, wakati akifungua semina kwa watia nia wa ubunge katika majimbo 19 ya Kanda ya Pwani iliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Aidha, aliwataka wananchi wote bila kujali itikadi ya vyama vyao kuhakikisha mgombea aliyeshinda uchaguzi anatangazwa kwa kutumia nguvu ya umma.

"Imejengeka desturi kwa wakurugenzi na wasimamizi wa uchaguzi kuchakachua matokeo na kumtangaza mtu ambaye hakushinda uchaguzi, jambo ambalo ni kinyume cha sheria, halikubaliki na linastahili kupingwa kwa nguvu ya umma," alisema na kuongeza:

"Natoa wito kwa wanachama hata wale ambao hawakutia nia waende kwenye ofisi za chama wakachukue fomu."

Kwa mujibu wa Mnyika, kutia nia ni jambo moja na kuchukua fomu ni jambo jingine, na kwamba ni vyema wanachama wakatumia fursa hiyo ili wateuliwe kuwahudumia wananchi.

"Natangaza rasmi kuwa uchaguzi wa mwaka huu ni uchaguzi wa nguvu ya umma. Wananchi wakapige kura kwa wingi wao na wahakikishe wanalinda ushindi wao kuanzia kwenye vituo vya kupigia kura mpaka kwenye vituo vya kujumlisha matokeo," alisema.

Julai 4, mwaka huu, CHADEMA ilianza utaratibu wa kuchukua fomu za kuwania nafasi za urais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, urais wa Zanzibar, ubunge na uwakilishi katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar.



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere (aliyekaa kulia), akisaidiwa kuangalia michango yake katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) wakati alipotembelea banda la mfuko huo kwenye Maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mti wa kimila wamweka matatani mtendaji kata

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

OFISA Mtendaji wa Kata ya Mvumi Makulu Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma, Happiness Pesa, amejikuta matatani baada ya kutoa kibali cha kukatwa na mti wa kimila uliokuwa unatumiwa na Chifu Mazengo.

Akizungumzia kuhusu tukio hilo, Chifu Mazengo wa pili, Henel Mazengo, alisema kitendo cha kukatwa kwa mti huo kumemwondolea mizimu yake aliyokuwa anaitumia kwenye kazi zake na hata alipojaribu kuwarudisha wamekataa kurudi kwa sababu nyumba yao imeharibiwa.

"Mimi ninachotaka ni watu wangu (mizimu) tu warudi kwa sababu hapa nilipo siwezi kufanya shughuli zozote za kichifu kwa sababu watu wangu hawapo," alidai.

Alipoulizwa kuhusu tukio hilo, ofisa huyo alisema alikuwa hajui kama mti huo unatumiwa kwa shughuli za kimila na kutoa kibali kwa mwananchi kukata mti huo kwa ajili ya shughuli zake za ujenzi.

Alisema kuna mwananchi, Joseph Paulo, ambaye alikwenda ofisini kwake kwa ajili ya kutaka kibali cha kukata mti kwa ajili ya shughuli za ujenzi.

"Nilipojiridhisha kuwa mwananchi huyo alikuwa amerhusiwa kujenga na mwenyekiti wa kijiji nilimpa kibali cha kukata mti huo, ambao sikujua kama unatumika kwa ajili ya shughuli za kimila."

"Lakini wakati mwananchi huyo anakata mti huo habari zilifika kwa ofisa tarafa ambaye alifika na kuzuia mti huo usikatwe kwa sababu unatumika kwa shughuli za kimila, lakini kwa sababu ulikuwa umeshaanza kukatwa ilibidi tawi lililokuwa linakatwa limaliziwe kukatwa," alisema Pesa

Alisema alimwita kwa Chifu Mazengo wa Pili ambapo alimtuhumu kukata mti huo na kusababisha mizimu yake kuhama na kutaka kuwarudisha watu hao, jambo ambalo alisema kuwa hawezi kulifanya.

Alisema Chifu huyo alisema kwenye mti huo kulikuwa na nyuki waliokuwa wanaishi humo ambao ni wa kimizimu, hivyo baada ya kukatwa mti huo wameondoka na yeye kutakiwa kuwarudisha kwani chifu huyo hawezi kufanya chochote hivi sasa baada ya nyuki hao kuondoka.

"Kwa kweli nilimwambia siwezi kuwarudisha nyuki hao kwa sababu sijui walipokwenda na kwa sababu siwezi kuwarudisha nimemwambia twende kwenye vyombo vya sheria wakatuamue kwa sababu tangu nimeanza kazi hapa sijawahi kuambiwa kuwa ule mti ni wa kimila na mwenye jukumu la kutuambia ni yeye chifu, lakini hakufanya hivyo mpaka haya yalipotokea," alisema Pesa.

HABARI KITAIFA

# Marufuku kuingiza kaya za watumishi wa umma TASAF

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WATENDAJI wa kata, vijiji na mitaa katika Manispaa ya Shinyanga, wameonywa kutoingiza kaya za watumishi wa serikali kwenye mpango wa kunusuru kaya maskini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) III Awamu ya Pili.

Badala yake wametakiwa waingize kaya ambazo ni lengwa ili zinufaike na fedha za TASAF na kuinuka kiuchumi.

Hayo yalibainishwa juzi na Mratibu wa Mpango wa Kunusuru Kaya maskini TASAF III awamu ya pili Manispaa ya Shinyanga, Octavina Kiwone, kwenye kikao kazi na watendaji wa kata, vijiji, na mitaa, kuwa wakati wa utambuzi wa kaya maskini linapoanza mara moja waingize kaya ambazo ni lengwa tu.

Alisema katika awamu iliyopita utambuzi wa kaya maskini haufanyika kwa weledi na uaminifu, ambapo ziliingizwa kaya hadi za watumishi wa serikali, jambo ambalo hataki kuliona katika awamu hii na atakayefanya hivyo atawajibishwa.

"Naombeni sana watendaji wa kata, vijiji na mitaa, mnapokwenda kuanza zoezi hili la kutambua kaya maskini, kalifanyeni kwa weledi na uaminifu," alisema na kuongeza:

"Hatutaki kusikia tena kuwapo na kaya za watumishi wa serikali kwenye TASAF, bali ingizeni kaya ambazo ni lengwa ili zinufaike na fedha na kuinuka kiuchumi."

"Mtendaji ambaye atakwenda kinyume cha maagizo ya serikali na kuingiza tena kaya ya mtumishi wa serikali au kuweka kaya hewa, mimi sipo tayari kutumbuliwa kwa uzembe wa mtu... lazima tutakushughulikia tu, nendeni mkafanye zoezi hili kwa uaminifu mkubwa na nadhani mnaifahamu serikali ya awamu ya tano haina mchezo," aliongeza.

Alitaja vigezo ambavyo kaya maskini inapaswa kuingizwa kwenye mpango huo wa TASAF, kuwa ni ile ambayo haina uwezo kabisa kwa kula milo mitatu kwa siku, uwezo wa kutotimizia mahitaji ya shule watoto, na kutopata huduma za kiafya. Mmoja wa watendaji hao, Mathias Masalu wa Mtaa wa Kunda Manispaa ya Shinyanga, waliahidi kwenda kulifanya zoezi hilo kwa weledi na uaminifu.




Wafanyakazi wa Hospitali ya St. Francis Ifakara mkoani Morogoro wakipokea msaada wa barakoa za kuwakinga na maambukizi ya Covid-19 zilizotolewa na kampuni ya bia ya TBL mwishoni mwa wiki. Aliyekabidhi msaada huo ni Mwakilishi wa Mauzo wa TBL Kanda ya Ifakara, David Mwamakula (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# PM ahimiza ujenzi Bandari ya Karema

**Na Neema Hussein,** KATAVI

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameweka jiwe la msingi kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Karema iliyopo katika Kata ya Karema wilayani Tanganyika mkoani Katavi, ambapo serikali imetenga Sh. bilioni 47.

Majaliwa aliweka jiwe hilo juzi huku akihimiza ujenzi huo ukamilike haraka.

Alisema kukamilika kwa bandari hiyo kutasaidia kukuza uchumi wa nchi kutokana na biashara za usafirishaji wa mizigo na abiria kutoka Tanzania kuelekea nchi jirani kama Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Burundi na Zambia. Majaliwa pia alizindua jengo la biashara liliojengwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na kupewa jina la Mpanda Plaza, ambapo alisema jengo hilo limeleta taswira mpya ya mji wa Mpanda.

Alilipongeza shirika hilo kwa ubunifu wao wa kujenga majengo hayo sehemu mbalimbali za mikoa ya Tanzania na pia alisisitiza majengo hayo yajengwe karibia nchi nzima ikiwezekana watafute soko la ujenzi nchi za nje.

Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Maulid Banyani, alisema katika mwaka huu wa fedha shirika hilo linatarajia kujenga majengo kama hayo katika mikoa wa Lindi na Kagera.

Majaliwa pia alizindua soko la pamba katika Chama cha Msingi cha Ushirika katika Kata ya Kasekese mkoani Katavi na kusema kuwa mwaka huu soko la pamba limeshuka kutokana na ugonjwa wa corona. Alisema wanunuzi wengi wa pamba hutoka nchi za nje, bei kushuka kutoka Sh. 1,200 kwa kilo hadi Sh. 810.

Kwa upande wao wakulima wa zao la pamba mkoani humo waliiomba serikali kuwapa elimu ya utumiaji wa mizani ya kupimia pamba, ili na wao waweze kujua namna ya upimaji kuepuka kuibiwa pointi zinazozidi katika kilo.

## Red Cross yasisitiza jamii kusaidia majanga

**Na Enock Charles**

CHAMA cha Msalaba Mwekundu Tanzania (Red Cross) kimewaomba wananchi kujitokeza kujitolea katika kazi mbalimbali za chama hicho ikiwamo kujitolea damu, ili kuwasaidia wengine wanapokumbwa na madhila.

Akizungumza wakati wa ugawaji wa vifaa mbalimbali kwa wawakilishi wa chama hicho katika baadhi ya mikoa nchini, Rais wa chama hicho Tanzania, David Kihenzile, alisema upo umuhimu na uhitaji wa watu kujitolea kuwasaidia wengine.

"Wito wetu kwa wadau ni kuungana na hii movement (harakati) yetu watakaoweza kusaidia katika huduma mbalimbali kwa nchi kama Tanzania yenye watu karibuni milioni 55 tulitamani angalau asilimia 10 ya Watanzania wajitolee," alisema Kihenzile.

Akikabidhi vifaa hivyo kwa baadhi ya mikoa ikiwamo Dar es Salaam na Pwani, alisema vina thamani ya Sh. milioni 54 ambavyo ni jenereta, simu na vifaa vya kuunganisha intaneti ili kusaidia katika kazi za uokoaji, huku pia akizindua namba maalum ya wananchi kupiga ili kupata msaada wa haraka bure ambayo ni 0800750150.

Alisema wakipatikana watu wengi watakaojitolea baadhi ya shida zitapata suluhisho kwa haraka akitolea mfano ya kwamba uhaba wa damu katika hospitali nyingi nchini utapungua.

Mwenyekiti wa chama hicho Mkoa wa Dar es Salaam, Rajab Senge, alisema vifaa hivyo vitasaidia kazi mbalimbali kufanyika kwa wakati na kutoa huduma kwa haraka kwa wananchi tofauti na ilivyokuwa awali.

## Waishukuru jumuiya kuwajengea visima

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANANCHI wa kijiji na kata ya Nyandekwa, Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga, wameipongeza Jumuiya ya International Istiqaama Muslimu Community ya Omani kwa kujenga visima virefu sita vya majisafi na salama kwenye vijiji sita na kuondoa tatizo la ukosefu wa huduma hiyo.

Pongezi hizo walizibainisha jana wakati wa uzinduzi wa visima hivyo vyenye urefu wa mita 15 kwenda chini, vilivyojengwa kwa ufadhili wa jumuiya hiyo, ambapo walisema kata hiyo ina visima virefu vilivyojengwa na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere tangu mwaka 1970, lakini havitoshelezi mahitaji.

Ester Joseph, mkazi wa Kata ya Nyandekwa, alisema awali walikuwa wakifuata huduma ya maji kwenye kata jirani kwa zaidi ya kilometa tatu na walipokuwa wakichelewa kurejea majumbani walikuwa wakiadhibiwa na waume zao kwa kulalamikiwa wanasaliti ndoa.

# IATA yatoa ithibati kwa NIT kutoa kozi 4 usafiri wa anga

**Na Prosper Makene**

SHIRIKA la Kimataifa la Usafiri wa Anga (IATA), limetoa ithibati kwa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kuanza kutoa kozi nne za usafiri wa anga, ambapo zitaanza kutolewa katika mwaka wa masomo 2020/21.

Kozi hizo ambazo zitatolewa na shule Kuu ya Teknolojia ya Usafiri wa Anga katika chuo hicho ni pamoja na “Airline Customer Service”, “Airline Marketing”, “Global Distribution Systems Fares and Ticketing-Amadeus” “Airport Operations Fundamentals”.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Zacharia Mganilwa, aliwaambia wanahabari jijini Dar es Salaam kuwa; “Tumepata ithibati kutoka IATA kutoa kozi nne katika sekta ya usafiri wa anga baada ya kukidhi vigezo na kusaini mkataba wa makubaliano mwezi Machi mwaka huu.”

Prof. Mganilwa alisema wamekamilisha kulipa malipo ya ada ya usajili kwa IATA, na maandalizi ya kuanza kutangaza kozi hizo.

Prof. Mganilwa aliongeza: “Baada ya kuanza kutoa kozi kama hizi za IATA hapa chuoni, Watanzania watapata fursa ya kusoma kozi za kimataifa zinazo tambulika kwa gharama nafuu.”

Alisema hatua hiyo itawasaidia wahitimu wa kozi hizo kupata fursa za ajira kwa urahisi katika kampuni za ndege na katika viwanja vya ndege nchini na duniani.

“Baada ya kupata idhini ya kuendesha mafunzo ya kozi hizi kutoka IATA, tunawakaribisha watu binafsi na mashirika ya ndege ya ndani na nje ya nchi kuleta wafanyakazi wao kusoma kozi hizi. Masomo haya yatawaongezea maarifa na umahiri bora katika maeneo yao ya kazi katika sekta ya usafiri wa anga,” alisema. Alisema chuo kina mipango zaidi ya kuongeza kozi zenye tija kutoka Shirika hilo la Kimataifa (IATA) ili kupata wataalamu stahiki watakaoboresha huduma katika sekta ya usafiri wa anga ndani na nje ya nchi.

Vile vile, Profesa Mganilwa amebainisha kuwa wataanza kutoa kozi ya urubani ambapo tayari wamepokea dola milioni 21.25 za Kimarekani (Sh. nilioni 50) kutoka Benki ya Dunia WB kwa ajili ya ununuzi wa ndege tatu za mafunzo, vifaa vya kufundishia wahandisi wa ndege kujenga karakana na hosteli.

Mkuu wa Shule Kuu ya Teknolojia ya Usafiri wa Anga katika Chuo hicho, Denis Mwageni, alisema taasisi hiyo ilianza kutoa kozi za uhandisi wa matengenezo ya ndege mwaka wa masomo 2015/16.



Wahitimu wa kozi ya uhudumu wa ndege katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kilichopo jijini Dar es Salaam wakiwa kwenye mahafali hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mhadhiri aeleza umuhimu mafunzo ya uongozi, maadili

**Na Romana Mallya**

MHADHIRI wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kilichopo Kigamboni, jijini Dar es Salaam, Dk. Samuel Nyulelele, amesema mafunzo ya uongozi na maadili ni muhimu hasa kipindi hiki taifa linapoelekea katika uchumi wa viwanda, sayansi za uzalishaji na usindikaji ili kupata watu wenye nidhamu kazini.

Dk. Nyulelele ambaye ni msimamizi wa washiriki katika chuo hicho kwenye Maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa, akizungumza katika viwanja vya Sabasaba jana, alisema chuo hicho kinatoa mafunzo hayo ili kuwaandaa viongozi wajao na waliopo madarakani kuwa na nidhamu.

Alisema mafunzo hayo ya uongozi na maadili yanalenga makundi tofauti chuoni hapo.

“Lengo la mafunzo haya yanasaidia kurekebisha mwenendo wa mtu kurudi katika mstari atakapoanza kutumikia taifa,” alisema.

Alisema kihistoria viongozi wengi wamepitia chuoni hapo nao wanatoa ushuhuda kuwa mafunzo hayo yana manufaa.

“Kiongozi mwenye nidhamu uzalishaji wake utakuwa bora kwamba ataweza kufanya kazi kwa kujituma kwa kuzingatia maadili,” alisema.

Alisema katika maonyesho hayo, chuo hicho kipo kwa ajili ya kuelimisha umma kuhusu majukumu mbalimbali ambayo chuo kimekuwa kikifanya na kuendelea kuyafanya.

Akielezea historia ya chuo hicho alisema kilianza kabla ya uhuru lengo likiwa ni kufundisha viongozi ambao wangeweza kushika madaraka katika Tanganyika huru.

“Hata baada ya uhuru chuo kiliendelea kuandaa viongozi, lakini wale ambao wanazingatia zile tunu za taifa za wakati huo na mwasisi wa chuo ni Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa kwanza wa taifa la Tanganyika.

Alisema kwa sasa chuo kimejikita kwenye mafunzo baada ya mabadiliko kadhaa yaliyotokea mwaka 2005.

Alisema sheria ya chuo ilikielekeza pamoja na masomo mengine na taalamu nyinginezo kuwe na utoaji wa mafunzo ya maadili na uongozi ambalo ndio chimbuko lake.

# Serikali yapongeza mageuzi ya BRELA

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameupongeza Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), kwa namna ilivyofanya mageuzi ya kuboresha huduma zake katika kipindi kifupi.

Alitoa pongezi hizo mwishoni mwa wiki alipotembelea banda la BRELA kwenye Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara yanayoendelea kwenye viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.

“Sikutarajia kushuhudia mteja akifanya usajili na kupata cheti chake hapa, hakika hii ni hatua kubwa mmefikia katika kuhakikisha kwamba mnatengeneza mazingira mazuri kwa wafanyabiashara hapa nchini ili waweze kurasimisha biashara zao,” alisema Majaliwa.

Awali, Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, aliitaka BRELA pamoja na taasisi zingine zilizo chini ya wizara yake kuboresha mikakati yake ya kuwafikia wananchi katika halmashauri zao.

Alisema ni muhimu kwa BRELA pamoja na taasisi zilizo chini ya wizara yake kuhakikisha zinaboresha mikakati ya utoaji wa huduma na kuyatumia maonyesho hayo kama fursa.

Awali, Ofisa Mtendaji Mkuu wa wakala huo, Godfrey Nyaisa, alisema lengo kuu la kushiriki katika maonyesho hayo ni kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma na utatuzi wa changamoto zao zote papo kwa papo.

“Tunataka wananchi watambue kwamba BRELA ya sasa siyo kama ile ya zamani, mambo yamebadilika na tuko hapa leo kudhihirisha hilo kwa utoaji wa huduma za papo kwa hapo,” alisema.

Alisema wako kwenye maonyesho hayo kwa ajili ya kujibu hoja za wananchi ana kwa ana, kutoa elimu kuhusu huduma wanazotoa na kuelezea kwa namna gani hivi sasa taasisi hiyo imeboresha mifumo yake.

“Ni wito wangu kwa kila wananchi wanaohitaji huduma za BRELA kufika katika banda letu lililopo ndani ya banda la Wizara ya Viwanda na Biashara ili wapate huduma zozote wanazohitaji hapo hapo,” alisema Nyaisa.

Nipashe
Spotika



MAKOCHA 9 WANAOWEZA KUMRITHI SETIÉN BARCELONA UK. 12&13



# SANE ALIVYOTUA KIBABE BAYERN

**MUNICH,** Ujerumani

KLABU ya Bayern Munich imekamilisha usajili wa winga, Leroy Sane kutoka Manchester City.

Sane mwenye umri wa miaka 24, amekubali kusaini mkataba wa miaka mitano na miamba hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, ambao walithibitisha usajili wao Ijumaa iliyopita.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani kwa awali ameigharimu Bayern euro milioni 49, na itapanda hadi euro milioni 60, kwa mujibu wa Stats Perform News.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bayern, Karl-Heinz Rummenigge, baada ya usajili huo alisema: "Tuna furaha kubwa kumkaribisha Leroy Sane hapa FC Bayern. Ni mmoja wa wachezaji ambaye tunamwelewa na ameshajithibitishia ubora wake mwenyewe kwa miaka michache iliyopita, hasa akiwa na timu ya taifa.

"Malengo yetu ni kuwaleta wachezaji bora wa Ujerumani hapa FC Bayern na usajili wa Leroy unahimiza malengo yetu. Ningependa kumshukuru Hasan Salihamidzic kwa kufanikisha uhamisho wake."

Salihamidzic, Mkurugenzi wa Michezo wa Bayern, aliongeza: "Tumefurahia ujio wa Leroy na kuwa mchezaji wetu wa Bayern. Leroy ni mtu wa kutengeneza tofauti na ataweza kuiimarisha timu yetu.

"Kwa uwapo wa Serge Gnabry, Kingsley Coman na Leroy, sasa tuko bora zaidi na tuna vifaa bora kuvitumia katika kila nafasi na ni watu muhimu sana kwenye kikosi chetu.

"Ningependa kuishukuru Manchester City kwa kuelewa na kufikia makubaliano mazuri. Ningependa pia kumshukuru rais na mwenyekiti kwa kuisimamia vizuri bodi ya wakurugenzi, Herbert Hainer, ambaye alikuwa mbele kwenye usajili huu tangu mwanzo na alielewa matatizo ya mlipuko wa virusi vya corona."

Akizungumza kabla ya mchezo wa Jumatano, Pep Guardiola alimtakia kila la heri mchezaji huyo kwa kile alichokifanya pale City na akasema ni mchezaji "sahihi" kwa Bayern.

Sane kujiunga na Bayern lilikuwa suala la muda tu, kwa sababu alikuwa akifuatiliwa tangu mwaka jana, ingawa awali miamba hao wa Ujerumani walibainisha kwamba wasingeweza kufikia bei waliyokuwa wakitaka City.

Halafu akakumbwa na majeruhi makubwa ya goti wakati wa mchezo wa Ngao ya Jamii Agosti, mwaka jana na amerudi uwanjani mwezi uliopita.

Sane alijiunga na City akitokea Schalke mwaka 2016 katika dili ambalo lilitajwa kuwa thamani yake ni pauni milioni 37 na alikwenda kuonyesha kipaji cha kuvutia katika msimu wake wa kwanza.

Msimu wa 2017/18 alishinda tuzo ya mchezaji bora kijana wa mwaka wakati kikosi cha hicho cha Guardiola kikitwaa taji la Ligi Kuu England. Sane aliisaidia City kutwaa taji hilo tena msimu uliofuata huku yeye mwenyewe akifunga mabao 16 katika mashindano yote, na hapo akaanza kuhusishwa na mpango wa kuwaniwa na Bayern.


Msimu huu kwa muda mwingine, Sane ameutumia akiwa majeruhi na kule Bayern ndio haswa sasa anakwenda kuonyesha kipaji chake kwa msimu unaokuja.

Guardiola amekubali kumuuza Sane kwa sababu angemwachia maana yake angeondoka kama mchezaji huru, kwani mkataba wake uliokuwa unamalizika Juni 2021.

Sasa Bayern, kwa ujio wa Sane maana yake ameongezeka baada ya ujio wa Tanguy Kouassi kutoka Paris Saint-Germain, ambaye mkataba wake na mabingwa hao wa Ufaransa ukiwa umemalizika.

## ISIKUPITE

KIUNGO mkongwe wa Barcelona, Xavi Hernandez, anatajwa kuwa mmoja wa makocha wenye nafasi kubwa ya kurithi mikoba ya Quique Setien, ambaye amekalia kuti kavu ndani ya Nou Camp baada ya vigogo hao wa Hispania kupoteza pointi sita kwenye mechi sita tangu La Liga iliporejea.



## Extra Time



# MAKOCHA 9 WANAOWEZA KUMRITHI SETIÉN BARCA

**BARCELONA,** Hispania

HUKU msimu ukielekea ukingoni, muda huu sio mzuri kwa Kocha wa Barcelona, Quique Setién.

Barcelona imeanguka tangu kurudi tena kwa LaLiga, imeiruhusu Real Madrid kuwa juu kwenye mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Hispania.

**Soka lao halivutii na wachezaji wanaonekana kutokuwa kwenye viwango vyao na inaonekana mambo ni mabaya na Setien anaweza kufukuzwa mara tu baada ya msimu huu kufika mwisho.**

Hapa tunawaangalia makocha 9 ambao wanapewa nafasi ya kuchukua mikoba yake.

### 1. MAURICIO POCHETTINO

Mauricio Pochettino pengine ndio mtu ambaye anaweza kuwa kwenye nafasi kubwa zaidi ya kupewa mikoba hiyo, kwani hana kibarua chochote kwa sasa.

Anaweza kuwa mtu mzuri zaidi kwa nafasi hiyo, ingawa alishawahi kusema kwamba anaweza asiende pale Camp Nou kwa sababu alishawanoa wapinzani wao wakubwa wa Barcelona pale Katalunya, Espanyol.

### 2. EUSEBIO SACRISTAN

Eusebio Sacristán alishinda mataji manne ya LaLiga kama mchezaji akiwa na Barcelona kabla ya kutumia miaka minne kufundisha kikosi B kati ya mwaka 2011 na 2015.

Pia alikuwa sehemu ya benchi la ufundi chini ya Frank Rijkaard pale Camp Nou. Kama Barça wanamtaka mtu anayeielewa vizuri klabu hiyo, Eusebio ndio mtu anayefaa kwa kazi hiyo.

Hata hivyo, tatizo la Eusebio hajawahi kuwa na mafanikio nje ya Barcelona. Alifanya kazi pale Real Sociedad na kwa sasa hana kazi tangu kipindi cha majira ya joto kilichopita, wakati timu yake ya Girona iliposhuka daraja.

Hajawa na rekodi ya kuvutia nje ya Barcelona, hivyo kazi hii inaweza kuwa kubwa zaidi kwake.

### 3. XAVI HERNANDEZ

Xavi anataka kurudi Barcelona? Ndio.

Wao Barcelona wanamtaka arudi? Ndio, walijaribu kumtaka kabla ya Setien.

Lakini ni ukweli uliowazi kwamba, Xavi hawezi kwenda pale Barcelona chini ya bodi ya wakurugenzi wa sasa na rais aliyepo.

### 4. ROBERTO MARTINEZ

Alionekana ndio mrithi wa Ernesto Valverde kabla ya ujio wa Setién, na jina la Roberto Martínez bado linazungumzwa katika viunga vya Barcelona kama ndio kocha ajaye.

Bado ana mkataba na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, lakini Martínez anaweza kuwa mtu sahihi zaidi kwa kikosi hicho. Yeye ni kocha mzuri, lakini rekodi zake hazionyeshi kama ndoto ya Barça.

Muda wake pale Everton ulimalizika kwa aina yake, na ingawa kikosi chake cha Ubelgiji kinafanya vizuri, anaweza kufikiriwa kutua Katalunya.

### 5. MASSIMILIANO ALLEGRI

Kocha wa zamani wa Juventus, Massimiliano Allegri inaaminiwa kwamba alikataa nafasi ya kujiunga na Barcelona, lakini uvumi haujakoma kumhusisha na kazi hiyo.

Akiwa ameshinda mataji matano ya Ligi Kuu Italia, Serie A, kwa jina lake, Allegri anaonekana ni mtu anayefaa kuchukua mikoba pale Barcelona, lakini staili yake inaonekana kutofiti pale kwenye dimba la Camp Nou.

Kikosi chake cha Juventus kilikuwa kinacheza soka la taratibu kitu ambacho ni kinyume na Barcelona. Anaweza kupewa mikoba hiyo kwa kufuata mfumo wa uchezaji wa kikosi hicho.

MAURICIO POCHETTINO

### 6. LUIS ENRIQUE

Akiwa ameshinda mataji matatu katika mwaka wake wa kwanza na mataji mawili mwaka uliofuata, Luis Enrique bado ana nafasi kubwa ya kuchukua mikoba ya Barcelona.

Mtazamo wake na aina ya uchezaji wa timu yake, ulileta kitu fulani cha kuvutia kwa kikosi hicho na bado Enrique kazi yake inathaminiwa pale Katalunya kwa kipindi cha miaka mitatu aliyokaa.

Kwa sasa ni kocha wa Timu ya Taifa ya Hispania, lakini Enrique hajawahi kuacha kuonyesha mapenzi yake kwa kikosi cha Barcelona, hivyo ana nafasi ya kurudi kwenye klabu hiyo na kuachia majukumu ya kulinoa taifa hilo.

### 7. RONALD KOEMAN

Ni gwiji wa Barcelona na Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Ronald Koeman na anapendwa zaidi na mashabiki wa pale Camp Nou, hivyo uwezekano wa kutua pale ni mkubwa zaidi kwa siku za usoni.

Koeman anaelewa njia zote za mfumo ulioasisiwa na Johan Cruyff na mara zote yupo tayari kujaribu kuendelea kuufanyia kazi. Kumiliki mpira na kuamini vijana ndio sehemu ya mfumo huo.

Muda wake pale Everton haukuwa mzuri, lakini amejenga heshima kubwa akiwa na Uholanzi. Na kuna uwezekano wa kupewa nafasi ya ukocha katika kikosi hicho.

### 8. MARCELO GALLARDO

Marcelo Gallardo bado hajajijaribu yeye mwenyewe barani Ulaya, lakini rekodi yake na kikosi cha River Plate cha kule Argentina ni ya kuvutia.

Kutokana na staili yake amekuwa mmoja wa makocha vijana maarufu sana na anajulikana pia pale Camp Nou, anapenda soka la kushambulia mwanzo mwisho na ameiwezesha timu yake kucheza soka la kuvutia zaidi.

Tatizo moja tu ni kwamba, hajawahi kuinoa timu yoyote barani Ulaya zaidi ya kuwa kule Amerika Kusini. César Luis Menotti na Gerardo Martino walishindwa kutamba walipojaribu kwenda Ulaya - je, Gallardo ataweza?

### 9. FRANCISCO GARCIA PIMIENTA

Inaonekana kama Barcelona wanasubiri tu muda wa kumpandisha kocha wa timu ya akiba, Francisco García Pimienta kwenye kikosi cha kwanza.

Anaonekana mmoja wa makocha wanaoufahamu vizuri mfumo wa timu pale Camp Nou, kwani Pimienta amekaa miaka 14 kwenye akademi ya klabu hiyo. Anajua namna ya kuwalea vijana wenye vipaji, na anauwezekano mkubwa akapandishwa kwenye kikosi cha wakubwa.

Kiukweli wengi wanamfananisha na Pep Guardiola, kwamba anafanana kwa vitu vingi na hasa ikichukuliwa kwamba naye alitokea kwenye kikosi B na kuja kutamba sana katika timu ya wakubwa. Wanaweza kutumia mfano huo kumpa mikoba ili kuiwezesha Barcelona kurudi kwenye nafasi yake.

## Nukuu

"Nawashukuru sana mashabiki wote, wafanyakazi na wachezaji wenzangu! Kila siku nitaendelea kukumbuka wakati mzuri tuliokuwa pamoja kwa furaha na kujivunia. Pia ninamshukuru kocha wangu (Pep Guardiola), kwa kunifanya kuwa mchezaji mzuri na kufikia kushinda tuzo ya Mchezaji Bora Chipukizi mwaka 2018. Nimejifunza vitu vingi na ninajivunia kuwa sehemu ya safari ya mafanikio." **Leroy Sane aliandika katika ukurasa wake wa Twitter baada ya kusajiliwa Bayern Munich.**



"Barcelona walinifuata mwaka 2017 kwa ajili ya kutaka kunisajili, ila niligoma kusaini dili lao kwa sababu Paris St- Germain ilikataa kuniruhusu," **amesema Angel Di Maria, nyota wa zamani wa Manchester United alipokuwa akizungumza na gazeti la AS.**



"Lengo kubwa ni kuhakikisha taji la Ligi Kuu England linasalia Anfield, nina hakika kazi hii itafanikiwa kwa sababu nitatengeneza kikosi imara, hatutatetea taji msimu ujao, bali tutaushambulia ubingwa kuhakikisha tunaupata tena kwa kishindo kikubwa," **Kocha, Jurgen Klopp alisema baada ya kuipa ubingwa Liverpool.**






# MILIMA, MABONDE, TAMU SIMBA KUUSAKA UBINGWA

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Simba imetimiza ndoto yake ya kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya tatu mfululizo, kama ambavyo baadhi ya viongozi wake walikuwa wakijinasibu kuanzia mwanzo wa msimu huu wa 2019/20.

**Kazi hiyo ilikamilika rasmi Juni 28, mwaka huu ilipotoka sare ya bila kufungana na Tanzania Prisons kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya na kufikisha jumla ya pointi 79 ambazo hakuna timu nyingine yoyote ambayo inaweza kufikisha.**

Simba ilitwaa ubingwa msimu wa 2017/18 na 2018/19 na ilikuwa ikihitaji tena msimu huu taji ili kulichukua kombe hilo moja kwa moja.

Haikuwa kazi rahisi msimu huu, kwani pamoja na Ligi Kuu msimu wa 2019/20 kuwa ngumu, lakini ilikabiliwa na changamoto ya mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19, unaosababisha na virusi vya corona ambao nusura uzime ndoto zao.

Karibu dunia nzima ilisimamisha michezo, huku baadhi ya nchi zikifuta kabisa ligi, hivyo kutokuwa na mabingwa msimu huu, badala yake kuteua wawakilishi kwenye mechi za kimataifa.

Hata hivyo ligi ilirejea na Simba kutimiza ndoto zake. Ndani ya uwanja pia hakukuwa na lelemama, kwani ilibidi ipigane na kutoa machozi, jasho na damu, ikipitia njia nzuri na ngumu, tambarare, milima na mabonde na kupata ilichokitaka.

Kwenye makala haya tunaangalia safari nzima ya Simba kuelekea kwenye ubingwa ilivyoanza hadi ilipoishia na jinsi ilivyokuwa ikikusanya pointi zake mwezi hadi mwezi.

### AGOSTI POINTI TATU

Simba ilianza kampeni yake ya kutwaa ubingwa msimu huu kwa kuvuna pointi tatu katika mechi yake moja iliyochezwa Agosti 29, mwaka jana.

Mechi hiyo ilikuwa ni dhidi ya Maafande wa JKT Tanzania na ilimalizika ikipata ushindi wa mabao 3-1, ikichezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam. Ilikuwa ndiyo mechi pekee iliyochezwa mwezi huo.

### SEPTEMBA POINTI TISA

Mwezi uliofuata, Simba ilicheza mechi tatu na ilishinda zote, ikikusanya jumla ya pointi tisa.

Ilianza kwa kuinyuka Mtibwa Sugar jijini Septemba 13, mwaka jana, ikiwa mjini Bukoba iliisasambua Kagera Sugar mabao 3-0 Septemba 26, na siku tatu baadaye, Septemba 29, iliiadhibu Biashara United ya Mara mabao 2-0.

### OKTOBA POINTI SITA

Mabingwa hao wa Ligi Kuu Bara walicheza mechi tatu Oktoba, lakini safari hii ikikusanya pointi sita tu, baada ya kushinda mbili na kupoteza mechi moja.

Ilikuwa ni baada ya kuichapa Azam FC bao 1-0, Oktoba 23, mwaka jana na ikashinda goli 1-0, Oktoba 27, mwaka jana dhidi ya Singida United jijini Arusha ambako timu hiyo ilihamia kwa muda, kabla ya kukubali kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Mwadui FC, Oktoba 30, mwaka jana, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kambarage, Shinyanga.

### NOVEMBA POINTI SABA

Ni mwezi ambao Simba ilivuna pointi saba baada ya kushinda mechi mbili na sare moja.

Zilipatikana kwa kuichapa Mbeya City mabao 4-0 Novemba 2, mwaka jana, ikalazimishwa sare ya bila kufungana dhidi ya Tanzania Prisons Novemba 7, mwaka jana kabla ya kuiangamiza Ruvu Shooting mabao 3-0 Novemba 23, mechi zote zikichezwa.

### DESEMBA POINTI TISA

Ilikuwa ni sikukuu ya Krismasi, Simba ilipotoa zawadi kwa mashabiki wake kwa kuichapa Lipuli mabao 4-0 hapa jijini na kama vile haikutosha, Desemba 28, mwaka jana ikaifunga KMC mabao 2-0, huku Desemba 31, mwaka jana ikishinda mabao 2-0 dhidi ya Ndanda FC, mechi zote zikichezwa Dar es Salaam.

### JANUARI POINTI 10

Shughuli ilianzia mwaka 2020, mwezi wa kwanza au Januari. Ni mwezi ambao ilikusanya pointi 10 na kusafisha kabisa njia ya kuutwa ubingwa.

Ilikuwa ni Januari 4, mwaka huu ilipoanza kwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Yanga, lakini ikaenda Mwanza na kuichapa Mbao FC mabao 2-1, Januari 16, siku tatu baadaye, Januari 19, iliiadhibi Alliance FC mabao 4-1, na Januari 29, ilitoa kipigo cha mabao 3-2 dhidi ya Namungo FC.

### FEBRUARI POINTI 18

Kwa kawaida Februari ni mwezi mfupi, lakini kwa Simba ndiyo mwezi iliyokusanya pointi nyingi zaidi kuliko miezi mingine msimu huu. Ilikusanya jumla ya pointi 18, ikicheza mechi saba.

Ilichapa Coastal Union mabao 2-0 Februari Mosi, kabla ya kuidungua Polisi Tanzania mabao 2-1 Februari 4, lakini ilipoteza mechi kwa kufungwa bao 1-0 dhidi ya JKT Tanzania Februari 7, mwaka huu.

Baada ya hapo, Februari 11 iliifunga Mtibwa Sugar mabao 3-0, huku iliichapa Lipuli bao 1-0 mjini Iringa Februari 15, mwaka huu na baadaye Februari 18 iliichapa Kagera Sugar bao 1-0 ikiwa mwenyeji na ilishinda mabao 2-0 dhidi ya Biashara Februari 22, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa.

### MACHI POINTI TISA

Simba ilifanikiwa kukusanya pointi tisa katika kipindi cha Machi baada ya kushuka dimbani mara nne.Machi Mosi, mwaka huu iliifunga KMC mabao 2-0, halafu Machi 4, mwaka huu ikaiadhibu Azam FC mabao 3-2, kabla ya kufungwa na Yanga bao 1-0 Machi 8, mwaka huu, ambapo Bernard Morrison alifunga goli hilo pekee. Ilijipoza kwa kuisasambua Singida United mabao 8-0 Machi 11, mwaka huu.

### JUNI POINTI NANE

Baada corona, Ligi Kuu iliruhusiwa tena mwezi Juni, na Simba iliingia na moto na kukusanya jumla ya pointi nane zilizoweza kuipatia ubingwa wa Tanzania Bara kwa msimu wa 2019/20.

Ilianza kwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Ruvu Shooting Juni 14, mwaka huu na Juni 20 iliichapa Mwadui mabao 3-0, ikashinda mabao 2-0 dhidi ya Mbeya City Juni 24 na Juni 28 ikapata sare ya bila kufungana dhidi ya Prisons.

### JE, WAJUA?




MSHAMBULIAJI wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Antoine Griezmann (29), anapambana kuhakikisha vigogo hao wa Hispania wanampa ruhusa ya kujiunga na Arsenal au Inter Milan ya Italia katika msimu ujao.





# Wauza mboga, matunda sasa wapata eneo rasmi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAFANYABIASHARA wa mboga na matunda zaidi ya 100, waliokuwa wanapanga bidhaa zao kwenye eneo hatarishi la kituo cha daladala Sabasaba jijini Dodoma, wameondokana na adha hiyo baada ya kupatiwa eneo rasmi la kufanyia biashara.

Eneo hilo walilopatiwa lipo ndani ya soko la Sabasaba.

Akizungumza na wafanyabiashara hao, Ofisa Masoko wa jiji hilo, James Yuna, alisema kuwa wameamua kutoa eneo hilo ili kuondokana na adha waliyokuwa wakiipata.

"Eneo walilokuwa wakifanyia biashara lilikuwa hatari kwao wakati mwingine daladala zinakanyaga bidhaa zao, au kupanga eneo ambalo gari linatakiwa kuegeshwa na kuna siku mtu aligongwa na gari," alisema.

Yuna alisema pamoja na kusumbuliwa na magari, lakini usalama wao ni mdogo kutoka na shughuli nyingine zinazofanyika katika eneo la daladala.

"Eneo ambalo walikuwa wanatumia kuna shughuli za uchomaji wa mahindi, kukaanga chipsi kunaweza kusababisha mlipuko wa moto kutokana na magari kutumia nishati ya mafuta. "Mnang'ang'ania kubaki, sio salama kwa maisha yenu moto unaweza kulipuka na ukaleta maafa makubwa sana, lakini usumbufu wa magari kila wakati mnapanga bidhaa na kupangua ili tuu kupisha daladala zinazoingia na kutoka," alifanua Yuna.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Fatma Issa, alisema wanaishukuru Halmashauri ya Jiji la Dodoma, kwa kuwapatia eneo hilo ambalo watalitumia kufanya shughuli zao.

Alisema, awali pamoja na adha ya kusumbuliwa na magari, lakini pia eneo hilo halikuwa limefunikwa hivyo bidhaa zao kuharibika kwa jua pamoja na mvua hasa wakati wa masika. "Tunashukuru sana kwa kupata eneo hili kwani tulikuwa tunapata shida sana na bidhaa zetu hasa wakati wa mvua, sasa tunaomba uongozi wa soko, uhakikishe kuwa watu wote wanaondolewa kule ili wote tuje kufanya shughuli zetu hapa kwa pamoja," alisema.



Naibu Makamu Mkuu wa Chuo cha UDOM, Prof. Alexander Makulilo, akizungumza wakati wa kuzindua programu maalumu ijulikanayo Career Fair inayowawezesha wanafunzi wahitimu wa vyuo vikuu kupata ajira za muda kwenye benki ya NMB, uzinduzi huo ulifanyika mwisho wa wiki chuoni hapo jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# BAKWATA yamfagilia Magufuli Tanzania kuingia uchumi wa kati

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BARAZA Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Mkoa wa Dodoma, limesema jitihada za Rais John Magufuli za kudhibiti mapato na kutekeleza miradi mikubwa yenye tija, zimechangia Tanzania kuingia kwenye uchumi wa kati kwa kundi la chini.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mwenyekiti wa Halmashauri, Jafari Mwanyemba, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema kuwa kitendo cha Rais Magufuli, kudhibiti mapato yanayokusanywa na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimaendeleo.

"Hivi sasa kama Taifa hatusubiri watu kutoka nje waje watusaidie katika mambo yetu uwezo wetu wa kujitegemea umekuwa mkubwa tofauti na ilivyokuwa hapo nyuma," alisema Mwanyemba.

Alisema wakati ambapo Rais Magufuli, alichaguliwa, eneo la kwanza kufanya ziara ya kushtukiza ilikuwa ni katika Wizara ya Fedha ili kuona kama kuna watu wanaoweza kukifanya kile alichokusudia katika utawala wake.

"Pamoja na kudhibiti mapato, pia Rais amehakikisha kila Mtanzania anachapa kazi na kuacha kufanya kazi kwa mazoea hali ambayo imetusaidia kufika hapa ambapo leo Benki ya Dunia wanasema," alisema.

Pia, alisema katika sekta ya viwanda, Rais amesimamia vizuri na kusaidia kuongeza idadi ya ajira nchini pamoja na kuzalisha bidhaa na kusafirisha nje na kupata fedha za kigeni.

"Lakini kitendo cha kudhibiti rasilimali zetu pia kimesaidia sana kutufikisha hapa tulipo, mtakumbua hapo awali sakata la makinikia ambavyo lilikuwa na mvutano mkubwa, lakini leo limefanikisha hata kuzaliwa kwa kampuni ya Madini ya Twiga na kuongeza pato la taifa kupitia sekta ya madini," alisema.

Aliongeza: "Mimi sijawahi kuona kiongozi wa aina hii, ambaye anao uwezo wa kuona jambo, kubuni na kulitekeleza na kuleta ufanisi mkubwa kwa maslahi ya Watanzania wote."

Hata hivyo, alisema ni wakati sasa kwa wananchi kumlipa Rais Magufuli, kwa kile alichokifanya katika kipindi cha miaka mitano kwa kumpigia kura katika uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka huu.

"Hata vitabu vya dini vinasema kama mtu kakutendea jambo, basi unastahili umlipe, lakini kama huna uwezo basi unatakiwa kumpongeza," alieleza Mwanyemba.

## Wahitimu wa vyuo vikuu waonyeshwa fursa za ajira

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAHITIMU wa vyuo vikuu nchini wametakiwa kuchangamkia fursa za ajira zinazotangazwa kwenye maeneo mbalimbali na kuacha kutegemea kuajiriwa na serikali pekee.

Kauli hiyo ilitolewa na Naibu wa Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Prof. Alexander Makulilo, alipokuwa akifungua mafunzo na programu maalum ya Benki ya NMB iitwayo 'career fair' inayomwezesha mwanachuo wanaomaliza masomo kuomba ajira kwenye benki hiyo.

Prof. Makulilo aliwataka kuacha kukatishwa tamaa na wengine kwa kuwa ajira zipo na kinachotakiwa ni kujiandaa kuingia kwenye soko la ajira.

"Acheni kukatishwa tamaa na wengine, ajira zipo, waliohitimu miaka ya nyuma inawezekana hawakufanya vizuri katika masomo yao na ndio maana wanashindwa kupata ajira…fuatilieni matangazo ya nafasi za kazi zinazotangazwa mtapata ajira," alisema.

Alisema kichotakiwa ni masharti na vigezo vya ajira hizo kwa sababu kila idara inahitaji wasomi waliofanya vizuri kwenye masomo yao.

"Msome vizuri na muwe na ufaulu mzuri ili kuingia kwenye ushindani wa soko la ajira kwa sababu ajira zipo ila vigezo ndio muhimu kuzingatiwa," alisema.

Aliishukuru Benki ya NMB kwa kuwapelekea wahitimu wao fursa hiyo ya ajira.

Naye Meneja wa NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi, alisema benki hiyo inafanyakazi bila ubaguzi na kila mfanyakazi aliyepo kwenye ajira anatamani kuendelea kubaki kutokana na upendo na usawa unaoonyeshwa na viongozi na wafanyakazi wote.

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Rasilimali Watu wa Benki hiyo, Joanitha Rwegasira, alisema lengo la programu kwa wanafunzi ni kuwatangazia fursa za ajira pindi watakapomaliza masomo yao.

Rwegasira alibainisha kuwa wanachuo watakaoweza kupata nafasi hiyo ni wale wenye ufaulu wa kuanzia GPA ya 3.8 na wasiwe na umri zaidi ya miaka 25.

Alisema programu hiyo ni ya miaka miwili na watakaochaguliwa watafanyakazi kwa mwaka mmoja kwa matawi mbalimbali kwenye idara zote ili kujifunza na kuchagua idara itakayofaa kuanza nayo katika ajira.

Aidha, alisema benki hiyo ina wafanyakazi zaidi ya 3,000 nchi nzima na wanazingatia usawa wa kijinsia katika kuajiri kwao.





## Akamatwa kwa madai ya mauaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKAZI wa Kata ya Ilima katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, Upendo Anyimike (48), anashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani humo akituhumiwa kumuua, Sinaraha Mwang'onda (84).

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake juzi, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema mtuhumiwa alitekeleza tukio hilo Julai 2, mwaka huu, ambapo alimvamia marehemu nyumbani kwake na kumkata na kitu chenye ncha kali kichwani.

Alisema chanzo cha mauaji hayo ni mtuhumiwa kumtuhumu marehemu kuwa alimwibia pipa lenye thamani ya Sh. 20,000 na kutokomea nalo.

Kamanda Matei alisema baada ya mtuhumiwa kubaini kuibiwa pipa na marehemu, alimshtaki kwa Mwenyekiti wa Kijiji na marehemu alikiri kosa na kutakiwa kulipa Sh. 20,000 kama fidia ya pipa aliloiba, lakini marehemu hakutekeleza. "Baada ya marehemu kutolipa faini hiyo ndipo umauti ulimkuta. Jeshi la Polisi linatoa wito kwa wananchi kuacha kujichukulia sheria mkononi na kugharimu maisha ya watu wengine bila sababu za msingi, 20,000 inagharimu maisha ya mtu kweli," alihoji Matei.

Alisema mwili umehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Rungwe ya Makandana, na kwamba upelelezi wa tukio hilo unaendelea.

Katika tukio lingine, Kamanda Matei alisema jeshi hilo linamshikilia Mbeso Mwampozia (40), mkazi wa Kata ya Ikukwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kwa kosa la kukutwa na dawa za kulevya aina ya bangi yenye uzito wa kilo 10 na gramu 215.

Alisemwa mtuhumiwa alikamatwa Julai 2, mwaka huu saa 2:00 usiku katika Kitongoji cha Itende Juu.

# Vyuo vya VETA kujengwa kwenye halmashauri zote

**Na Nebart Msokwa,** ILEJE

SERIKALI imesema inakusudia kukamilisha ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi (VETA) katika mikoa na halmashauri zote nchini kufikia 2025 ili kuzalisha idadi kubwa ya raslimali watu wenye ujuzi, kwa ajili ya maendeleo endelevu ya viwanda.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alipokuwa anazindua Chuo cha VETA cha Wilaya ya Ileje mkoani Songwe ambacho kimejengwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Japan.

Alisema ili kutimiza azma hiyo serikali kupitia wizara inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi huo, na kwamba katika baadhi ya mikoa ujenzi wa vyuo hivyo unaendelea katika hatua tofauti tofauti na kwamba mikoa mingine tayari vyuo hivyo vilishakamilika.

Alisema kwa sasa ujenzi wa vyuo vya VETA vya mikoa unaendelea katika mikoa minne ya Rukwa kwa gharama Sh. bilioni 10, Mkoa wa Geita kwa Sh. bilioni 9.8, Mkoa wa Njombe kwa gharama ya Sh. bilioni 10 na katika Mkoa wa Kagera chuo kinajengwa kwa ufadhili wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa gharama ya Sh. bilioni 22.04. "Katika ngazi ya wilaya ujenzi wa vyuo hivi umekamilika katika wilaya 11 kikiwamo hiki cha Ileje ambacho nimekizindua hii leo, lakini ujenzi unaendelea katika wilaya za Newala, Kasulu, Nyasa, Ruangwa na Kongwa," alisema Prof. Ndalichako.

Aidha, Prof. Ndalichako alisema katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, serikali ilitenga Sh. bilioni 40 kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vya VETA katika halmashauri 25.

Aliwataka wazazi na walezi kuwapeleka vijana wao kwenye vyuo vilivyojengwa na serikali ili wapate ujuzi ambao utawawezesha kuajiriwa na kujiajiri wenyewe kwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Taifa ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Peter Maduki, alisema bodi hiyo inaendelea kuboresha elimu inayotolewa kwenye vyuo hivyo kwa kuajiri wakufunzi wenye weledi pamoja na kununua vifaa vya kisasa vya kufundishia.

Alisema mbali na vifaa, pia bodi hiyo inakusudia kubadili mtaala wa vyuo vya ufundi kwa kubadili lugha ya kufundishia kutoka lugha ya Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili ili kuwawezesha wanafunzi kuelewa wanachofundishwa.

"Tunalenga kupandisha ufaulu wa vijana wetu kutoka asilimia 69 za sasa mpaka kuanzia asilimia 80 na kuendelea, lakini mpaka sasa VETA imefikia asilimia 70 ya malengo ambayo tulikuwa tumejiwekea," alisema Maduki.

Mkurugenzi Mkuu wa VETA, Pancras Bujulu, alisema kabla ya Waziri Ndalichako kuzindua chuo cha VETA Ileje pia alikuwa ameshazindua Chuo cha Paramawe cha Wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa na baadhi ya vyuo vilivyopo katika mikoa ya Kigoma na Katavi.

Aliwataka wananchi wanaoishi karibu na vyuo hivyo kushirikiana na viongozi wa vyuo kulinda miundombinu ya vyuo hivyo ili kuhakikisha vinadumu kwa muda mrefu.

Aliiomba serikali na taasisi zake kuvitumia vyuo vya VETA kutekeleza miradi mbalimbali ili kuviwezesha vyuo hivyo kupata fedha ambazo zitaviwezesha kununua vifaa.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali mstaafu Nicodemus Mwangela, alisema vyuo vya VETA vinasaidia kukabiliana na tatizo la ajira kwa maelezo kuwa vijana wakipata ujuzi wanaweza wakajiajiri wenyewe. Alisema hata mafundi wa mitaani wanaruhusiwa kujiunga na vyuo vya VETA ili kujiongezea ujuzi, na kwamba kwa kufanya hivyo watakuwa mafundi bora ambao watakuwa na uwezo hata wa kujenga miradi ya serikali.




Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako (wapili kulia) na baadhi ya viongozi wa Mkoa wa Songwe na Mamlaka ya Usimamizi wa Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini (VETA), wakisikiliza maelezo ya mmoja wa wanafunzi wa fani ya umeme wa Chuo cha VETA cha Wilaya ya Ileje mkoani humo, mwishoni mwa wiki, wakati wa uzinduzi wa chuo hicho. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Kituo cha afya chaombewa huduma za barabara, umeme

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKOA wa Mbeya umeiomba Serikali Kuu kuboresha miundombinu ya barabara na umeme katika Kituo cha Afya cha Kata ya Ikukwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ili kuboresha upatikanaji wa huduma.

Ombi hilo lilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, mwishoni mwa wiki alipokuwa mgeni rasmi kwenye uzinduzi wa kituo hicho, ambacho kinatarajiwa kitasaidia kuondoa tatizo la wananchi wa kata hiyo kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za afya.

Chalamila alisema endapo miundombinu hiyo itaboreshwa, wananchi wa eneo hilo watakuwa wanapata huduma kwa usahihi na kwa wakati kwa maelezo kuwa kituo hicho ni kikubwa na zimebakia huduma chache kuwapo ili kiwe na hadhi sawa na hospitali ya wilaya.

"Lakini hapa hapana huduma ya uhakika ya maji, hivyo tuendelee kuiomba serikali itusaidie kuboresha miundombinu hii ili wananchi wetu wafurahie huduma hii ambayo walikuwa hawaipati kirahisi miaka iliyopita," alisema Chalamila.

Aliishukuru serikali kwa kutoa zaidi ya Sh. milioni 900 kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho, na kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ni miongoni mwa halmashauri zilizopata vituo vingi vya afya.

Aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza (CCM), alisema uzinduzi wa Kituo cha Afya Ikukwa umesaidia kuwapunguzia wananchi tatizo la kutembea umbali mrefu kufuata huduma hasa wajawazito.

Alisema baadhi ya wajawazito walikuwa wanalazimika kujifungulia njiani wakati wakisafiri kwenda katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Mbeya Ifisi ambayo ni umbali wa zaidi ya kilomita 90 kutoka katika kata hiyo.

"Nimewahi kushuhudia wajawazito wakiwa kwenye zahanati iliyopo jirani na kituo hiki kwa zaidi ya siku mbili wakisubiri kupata gari la kuwapeleka hospitali ya wilaya, nilipatwa na uchungu sana na nilikuwa nahofia maisha yao," alisema Njeza.

Alisema kitendo cha serikali kuamua kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho ni kuisaidia jamii ya kijiji hicho, kata yenyewe na zile zinazopaka na kata hiyo.

Nao baadhi ya wananchi wa kata hiyo walisema baada ya kuona hali ni mbaya, waliamua kuanza kuchangishana fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya na baadaye serikali ikaamua kuingilia kati baada ya kuona umuhimu wa kituo hicho.

Mary Manji, alisema awali wagonjwa walikuwa wanabebwa kwenye machela kutoka kwenye maeneo yao kwenda kwenye barabara kuu ya Mbalizi - Mkwajuni ili wapate gari ya kuwapeleka Ifisi.

Alisema kuna baadhi ya wagonjwa walikuwa wanapoteza maisha kutokana na umbali mrefu, hivyo kitendo cha serikali kujenga kituo hicho cha afya imepunguza tatizo la kutembea umbali mrefu.



# Uzalishaji mpunga ndani waongezeka maradufu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MTEKNOLOJIA wa mbegu kutoka Wakala wa Mbegu za Kilimo wa Serikali (ASA), Grace Matima, amesema uzalishaji wa ndani kwa zao la mpunga umeongezeka kutoka tani 581 hadi 1,436.

Hayo aliyaeleza mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na wakulima wa zao hilo katika mabonde ya mpunga ya Kibondemzungu na Mtwango, visiwani Zanzibar. Alisema hatua hiyo imefanikiwa kutokana na wakulima kulima kwa wingi zao hilo.

Alisema tangu kuanzishwa kwa ASA kumeongeza uzalishaji kutoka asilimia 3-9 na kusema kuwa ni faraja kubwa kufikia malengo.

Alisema serikali zote mbili zimekuwa zikishirikiana kuhakikisha wakulima wanapata mbegu bora na zenye tija ili kuwainua wakulima wa zao hilo kimaisha na familia zao.

"Uzalishaji wa mbegu bora umeongezeka, na uagizaji wa mpunga kutoka nje umepungua kwa asilimia 19, hivyo ni faraja kwetu kuona tumetimiza lengo letu," alisema Matima.

Vilevile, alisema Zanzibar kuna ongezeko kubwa la utumiaji wa mbegu kutoka tani 75 mpaka 248 kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2017-2019.

Meneja wa shamba la mbegu Kilangali Kilosa, Aneth Molela, alisema wameridhishwa na utumiaji wa mbegu Zanzibar na kuwapa matumaini ya kuongeza uzalishaji kutokana na kujengwa kwa miundombinu mipya.

Alisema, wataendelea na uzalishaji wa miundombinu kwa msaada wa Benki ya Dunia na kuamini kwamba utaongeza tija kwa kutoagiza chakula kutoka nje.

Alisema upokeaji wa mbegu unasaidia kutoa mchango wa uzalishaji ndani na kupunguza kutoka nje.



Mtaalamu wa mbegu kutoka Wakala wa Mbegu za Kilimo za Serikali (ASA), Grace David Matima, akizungumza na wakulima wa mpunga katika bonde la Kibondemzungu na Mtwango Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN ZANZIBAR**

# Vyama ushirika vyatoa ajira zaidi ya 20,000

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Maudline Cyrus Castico, amesema uwapo wa vyama vya ushirika umesaidia kutoa ajira kwa wananchi zaidi ya 21,702, Unguja na Pemba.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu Siku ya Ushirika Duniani, alisema kati ya wananchi hao vijana ni 7,687 wenye umri kati ya miaka 18-35, ikiwa ni sawa na asilimia 35.

Alisema hatua hiyo inadhihirisha kwamba lengo la serikali la kuona kuwa taasisi hizo ziko imara katika kuwaunganisha na kuwawezesha wananchi kubadili maisha yao kiuchumi na kijamii limefanikiwa.

Alisema kuwa chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, vyama hivyo vya ushirika vimeimarika na vipya zaidi ya 3,000 vya uzalishaji mali na utoaji huduma vimeanzishwa na kusimamiwa.

Kadhalika, upo ushahidi wa kutosha kuwa wanaushirika wengi wametimiza ndoto zao za kuimarisha huduma za jamii, zikiwamo huduma za makazi bora, elimu kwa watoto wao, huduma za nishati na kuanzisha miradi ya kiuchumi inayoongeza pato la mtu mmoja mmoja na familia zao.

Alisema, mitaji ya Saccos imeongezeka kufikia bilioni 14 sambamba na kuimarisha utoaji mikopo zaidi ya Sh. bilioni 24 kwa wanachama wao na hali ya marejesho inaendelea vizuri.

Alisema wizara yake inaendelea kusimamia mageuzi makubwa katika uendeshaji na usimamizi wa vyama vya ushirika kwa lengo la kuhakikisha mafanikio yaliyopatikana yanaendelezwa ili yalete tija kwa wanachama na wananchi kwa ujumla. Pia, katika maadhimisho hayo, sekta ya ushirika Zanzibar inashuhudia kuimarishwa kwa misingi ya kisera, sheria na kanuni zake zinazoongoza vyama vya ushirika vya aina zote.

Siku ya Ushirika Duniani huadhimishwa kila Jumamosi ya mwanzo ya mwezi Julai na ujumbe wa mwaka huu ni, 'Vyama vya ushirika kuhimili mabadiliko ya tabia ya nchi'.

# Vijana waaswa kutotumiwa na wanasiasa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

VIJANA wametakiwa kuacha tabia ya kutumika kwa kuwafaidisha wengine katika harakati za kisiasa na kutumia fursa ya uwezo wao kuongoza watu na kuleta mabadiliko katika jamii.

Akizungumza na Nipashe, mjumbe wa umoja wa ushiriki Tanzania, Bakar Hamad, alisema kuwa imekua ni mazoea uchaguzi uliopita vijana kuwa mstari wa mbele katika mikutano ya kampeni, lakini wengi wao hawaendi kupiga kura siku ya uchaguzi mkuu.

Alisema katika uchaguzi wa mwaka huu wamejiandaa kuwahamasisha vijana wasiwe wapiga shangwe bali wawe washiriki kamili wa kuchagua na kuchaguliwa.

Alisema baadhi ya vijana hupigwa na kupata ulemavu wa kudumu kwa sababu ya kujiingiza katika vitendo vya uvunjifu wa amani hasa katika kipindi cha uchaguzi.

Alisema wana matumaini kuwa katika uchaguzi wa mwaka huu vijana wengi wataenda kupiga kura kwa sababu wengi wao wameshajiandikisha katika daftari la kudumu la wapiga kura.

Aliwataka vijana kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ili na wao waweze kuchaguliwa badala ya kuwa wasindikizaji wa kwenda kuwachagua wengine.

Naye mwanaharakati wa masuala ya vijana, Harusi Mpatani, alisema watahakikisha wanatoa elimu kwa vijana kulinda na kudumisha amani ya nchi na kushiriki katika harakati za kisiasa bila kufanya vurugu za aina yoyote.

Alieleza kuwa matumaini yao kuwa katika uchaguzi wa mwaka huu vijana wengi watagombea nafasi za uongozi ili kwenda kuwasemea vijana wengine katika ngazi za uamuzi.

Kwa upande wake, Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Ushiriki Tanzania, Salma Saadat, alisema umoja huo utahakikisha katika uchaguzi wa mwaka huu kuna kuwa na ushirikishwaji wa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Alisema makundi hayo ya pembezoni yamekuwa yakiachwa nyuma kutokana na mitazamo mbalimbali ya jamii ikiwamo mifumo dume.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MATANGAZO MCHANGANYIKO**

**Anayehitaji kukodi gari Scania** Mende Tipper 8x4 kwa mkataba wa kudumu. Gari itakuwa tayari mwishoni mwa July 2020. Inafaa kwa miradi kama ya ujenzi wa au uchimbaji madini. Mawasiliano 0784-668-810.


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SCHOLASTICA DOMINIC LYIMO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 335 CDY TOYOTA HARRIER. Chassis namba ACU150002712. Engine namba 2AZ0308118.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya Polisi: KRT/RB/1468/2020.**

### KUPOTEA KWA CHETI



**ANISHA NUNGU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.311/0013 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia FORODHANI SEKONDARI mwaka 1998. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: DOO/BI/21/VOL XVIII/185.

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**FAIR DEAL AUTO PVT LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya BAJAJ BOXER yenye namba za usajili MC 371 BUP, Chassis No.MD2A21B9HWF94410, Engine No.PFZWHF46820.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: DOD/DOD/RB/504258/2020.


***Uza,***

***Chenye Thamani***

***Kubwa Kwa Kutangaza***

***Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Ndege zisizojulikana zaishambulia Libya

**TRIPOL,** Libya

NDEGE za kivita zisizojulikana zilikotoka zimeshambulia kambi ya jeshi la anga la serikali ya Tripoli usiku wa kuamkia jana.

Kambi hiyo iliwahi kudhibitiwa na Jeshi la Khalifa Khaftar kabla ya kukombolewa na Jeshi la Serikali ya Tripoli kwa msaada wa Uturuki.

Taarifa iliyotolewa na Jeshi la Libya (LNA) ilieleza kuwa ndege za kivita zimeshambulia usiku kambi ya jeshi la anga ambayo hivi karibuni ilikombolewa na wanajeshi wa serikali inayotambuliwa kimataifa kwa msaada wa Uturuki, baada ya kuvizidi nguvu vikosi vya wanajeshi kutoka Mashariki.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa mashambulizi hayo yamefanywa na ndege zisizojulikana.

Mkazi wa mji wa Zintan ulioko karibu na kambi hiyo alisema mlipuko ulisikika kutokea upande iliko kambi hiyo ya kijeshi ya Watiya.

Kambi hiyo ilikombolewa Mei na Jeshi la serikali ya mjini Tripoli (GNA) na kuonekana kuwa mwanzo wa kuporomoka ghafla kwa harakati za Jeshi la Khaftar za miezi 14 za kuwania kudhibiti mji mkuu Tripoli pamoja na kurudi kwake nyuma katika eneo la pwani na kuelekea katika maeneo mengine ya kuendeleza mapigano.

Taarifa zaidi kutoka Tripol zinaeleza kuwa usaidizi wa Uturuki ulikuwa muhimu kwa Serikali Kuu mjini humo katika kuwatimua wanajeshi wa LNA na kuzima harakati zao, kwamba yalifanyika mashambulizi ya angani na mashambulizi ya kutumia ndege zisizokuwa na rubani zilizolenga hasa ngome za Khaftar za usambazaji wa silaha pamoja na zile za kupanga harakati za kijeshi. **DW**

# Rwanda kufungua viwanja vya ndege Agosti Mosi

**KIGALI,** Rwanda

**Rwanda ilifunga shughuli zake za ndege Machi, mwaka huu na kufunguliwa tena kwa watalii wanaotumia ndege binafsi na kukodi Juni 17, 2020.**

SERIKALI ya Rwanda imetangaza kuwa itafungua tena viwanja vyake vya ndege kuanzia mwanzoni mwa Agosti, mwaka huu.

Taarifa iliyotolewa na Wizara ya Miundombinu ya Rwanda ilieleza kuwa: "Viwanja vya ndege vya Rwanda vitafungulia tena shughuli za ndege za abiria Agosti mosi, 2020".

Machi, mwaka huu Rwanda ilisitisha huduma zote za ndege zinazoingia na zinazotoka isipokuwa tu kwa ndege za kubeba mizigo na zinazotumika kwa hali ya dharura kwa sababu ya janga la virusi vya corona.

Katika taarifa hiyo, Wizara ya Miundombinu ilieleza kuwa abiria wote wakiwamo wale wanaounganisha safari zao kuelekea nchi zingine watahitajika kuonyesha kibali kinachothibitisha kwamba hawana virusi vya corona kutoka kwenye maabara iliyoidhinishwa.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa cheti hicho lazima kionyeshe kuwa msafiri alifanyiwa majaribio ndani ya saa 72 tangu alipoingia Rwanda.

"Kuhakikisha usalama na afya kwa abiria, wahudumu na wafanyakazi wengine, shughuli kwenye viwanja vya ndege zinazingatia miongozo ya Wizara ya Afya na mapendekezo kutoka kwa Baraza la Uimarishaji wa Shughuli za Ndege," taarifa hiyo ilieleza.

Aidha, wizara hiyo imeongeza kwamba abiria wanaoingia Rwanda watafanyiwa tena vipimo.

"Kwa abiria wanaoingia Rwanda, watafanyiwa tena vipimo pindi tu watakapowasili, huku matokeo yakitolewa ndani ya saa 24 na katika kipindi hicho watakuwa kwenye hoteli zilizotengwa kwa gharama zao wenyewe," serikali ilieleza.

Hatua hiyo ndiyo ya hivi karibuni kuchukuliwa na Rwanda katika kufungua uchumi wake kwa awamu baada ya tangazo la katikati ya Juni la kufungua shughuli za utalii na kuanza tena kwa safari za kimataifa kwa wanaotumia ndege za kukodi.

Rwanda ilifunga shughuli zake za ndege Machi, mwaka huu na kufunguliwa tena kwa watalii wanaotumia ndege binafsi na kukodi Juni 17, 2020.

Hatua hiyo imeiweka Rwanda mbele kati ya nchi za Uganda na Kenya ambazo bado hazijafungua shughuli zake za ndege. **BBC**



Rais wa Marekani, Donald Trump, akiinua mkono baada ya kuwasili katika sherehe za kuadhimisha Siku ya Uhuru wa Taifa hilo mjini Washington. **PICHA: AFP**

# Ufaransa yagoma kuchunguza kifo cha Habyarimana

**PARLIS,** Ufaransa

MAHAKAMA ya Rufani Ufaransa imekataa ombi la kufungua upya uchunguzi kuhusiana na mauaji ya aliyekuwa Rais wa Rwanda, mnamo mwaka 1994, Juvenal Habyarimana, ambayo yalichochea mauaji ya kimbari ya watu 800,000.

Kulingana na taarifa iliyotolewa na mawakili wa familia za wale waliouawa pamoja na Habyarimana wakati ndege yake ilipodunguliwa, wanatarajia kukatia rufani uamuzi huo wa Mahakama ya Ufaransa.

Mahakama hiyo iliombwa kupitia upya uamuzi uliotolewa mwaka 2018 wa kuachana na uchunguzi dhidi ya waliokuwa washirika tisa na wengine wa zamani wa Rais Paul Kagame, katika kesi ambayo ilitia doa uhusiano baina ya mataifa hayo mawili.

Ndege iliyokuwa imembeba Rais Habyarimana aliyetokea jamii ya Wahutu, ilidunguliwa mjini Kigali Aprili 6, 1994, hatua iliyoibua mauaji ya kimbari ya watu 800,000, hususani kutoka kabila ya Tutsi, lakini Wahutu waliokuwa na msimamo wa wastani waliuawa.

Rais wa Burundi, Cyprien Ntaryamira wa kabila ya Hutu pia aliuawa kufuatia shambulizi hilo la ndege hiyo iliyodunguliwa na wakati ilipokuwa njia kuelekea kutua mjini Kigali.

Uchunguzi dhidi ya mauaji hayo ulianzishwa nchini Ufaransa mnamo mwaka 1998, kufuatia malalamiko ya familia za wafanyakazi wa ndege hiyo ya Ufaransa.

Uchunguzi huo, awali uliwaangazia zaidi washirika wa Rais Kagame, Mtutsi aliyeongoza vuguvugu la waasi wa Chama cha Rwandan Patriotic Front (RPF) na hatimaye kuingia mamlakani baada ya kuuangusha utawala wa Kihutu.

Rais Kagame, ambaye ametawala Rwanda tangu mwaka 2000, alivunja mahusiano ya kidiplomasia na Ufaransa kati ya mwaka 2006 na 2009 baada ya Ufaransa kutoa waranti ya kukamatwa washirika wake.

Na mnamo mwaka 2012, ripoti iliyochapishwa na wataalamu kutoka Ufaransa, ilisema kombora hilo lilifyatuliwa kutoka kwenye kambi ya Kanombe iliyokuwa ikidhibitiwa na jeshi la Habyarimana, na kubadilisha mkondo wa uchunguzi.

Kigali ilisema kwamba uchunguzi huo ulithibitisha imani yake kwamba shambulizi hilo lilifanywa na Wahutu wenye itikadi kali walioamini kwamba Habyarimana alikuwa na msimamo ya wastani na aliyepinga mchakato wa amani wa Arusha uliokuwa ukiendelea wakati huo.

Wakati uchunguzi ukiwa bado unaendelea taratibu, Rais Kagame aliituhumu Ufaransa katika maadhimisho ya miaka 20 ya mauaji ya Kimbari mwaka 2014, kwa kuwa na jukumu la moja kwa moja kwenye mauaji hayo.

Novemba ilianzisha uchunguzi dhidi ya madai ya maofisa wa Ufaransa kuhusika na mauaji ya kimbari.

Ufaransa hata hivyo inakana madai hayo na mwaka jana, Rais Emmanuel Macron alitangaza kuundwa kwa jopo la wanahistoria na watafiti kuchunguza madai hayo. **DW**




# BAYERN YAJIPANGA KUMBAKISHA THIAGO

**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA Mkuu wa Bayern Munich, Hansi Flick ana matumaini ya kumshawishi Thiago Alcantara kubaki kwa mabingwa hao wa Ujerumani, wakati uvumi ukitawala anatakiwa na Liverpool.

Thiago ana mkataba hadi mwaka 2020/21, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania ameripotiwa kuwa njiani kueleka kwa mabingwa wapya wa Ligi Kuu England, Liverpool.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 29, alitokea benchi zikiwa zimesalia dakika tatu mpira kumalizika wakati Bayern ikiibuka na ushindi wa mabao 4-2 dhidi ya Bayer Leverkusen Jumamosi kwenye fainali ya Kombe la Ujerumani, DFB-Pokal.

Hata hivyo, Flick hajakata tamaa ya kumbakisha Thiago - ambaye aliwasili hapo akitokea Barcelona mwaka 2013 na tangu hapo ameshinda mataji saba ya Bundesliga.

"Mara zote kitu cha muhimu ni kuwa na matumaini. Mara zote nina mtazamo chanya zaidi kuhusu vitu," alisema Flick akiwaambia waandishi wa habari baada ya ushindi huo mjini Berlin.

"Pia najua bila shaka yoyote natakiwa kumbakisha mchezaji huyo wa Hispania, naamini hilo litawezekana.

"Ninajaribu kwa uwezo wangu wote kuhakikisha Thiago anabaki na nitamshawishi kubakia hapa. Na muda utaonyesha."

# Havertz anukia kutua Chelsea

**LONDON,** England

KAI Havertz, nyota wa Bayer Leverkusen anatajwa kuibukia ndani ya Chelsea msimu ujao baada ya makubaliano yaliyofanyika na kiongozi wa masuala ya michezo, Rudi Voller ndani ya klabu hiyo.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 21, amehusika kwenye jumla ya mabao 23 ndani ya klabu hiyo akifunga mabao 15 na kutoa pasi za mwisho nane.

Kiongozi huyo amesema kuwa makubaliano ambayo yamewekwa iwapo yatatimia basi nyota huyo atakipiga ndani ya Chelsea msimu ujao.

Kiungo huyo mwenye uwezo mkubwa ndani ya uwanja, Bayern Munich ambao ni mabingwa wa Bundesliga walikuwa wanahitaji saini yake ila wameamua kujiweka kando baada ya kuona kwamba kinda huyo anapenda kwenda Chelsea.

"Kwa sasa bado ni mchezaji wetu na tuna mipango naye ila tuna matumaini kwamba anaweza kubaki hapa kwa muda, akihitaji kuondoka hakuna tatizo hatuwezi kumzuia," amesema.






# Van Dijk: Klopp alinifanya niipende zaidi Liverpool

**LIVERPOOL,** England

VIRGIL van Dijk amebainisha kuwa, Jurgen Klopp ndio ilikuwa sababu kubwa kwa yeye kujiunga na Liverpool badala ya Manchester City au Chelsea.

Mlinzi huo wa kati aliondoka Southampton kwenda Anfield Januari, mwaka 2018 kwa ada iliyoripotiwa kuwa ni pauni milioni 75, ambayo iliweka rekodi ya beki ghali zaidi.

Kulikuwa na sehemu nyingine ambayo Van Dijk alikuwa akiwaniwa, City na Chelsea, lakini raia huyo wa Uholanzi aliamua kuwachagua wekundu hao wa kwa sababu ya uwepo wa Klopp, ambaye ameiongoza Liverpool kwenye taji lake la kwanza la Ligi Kuu England msimu huu.

"Nilikuwa na nafasi ya kwenda Chelsea na City," amesema Van Dijk akinukuliwa na magazeti ya Uingereza.

"Wakati unapolinganisha klabu, unaangalia historia, mji, kikosi cha sasa na mipango ya baadaye.

Van Dijk mwenye umri wa miaka 28, tayari ameshatwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, UEFA Super na Klabu Bingwa ya Dunia akiwa mchezaji wa Liverpool.

# Mourinho ajiandaa kumkumbatia Ancelotti

**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho amesema amejiandaa kuvunja sheria ya kukaa mbali ili aweze kumkumbatia Kocha wa Everton, Carlo Ancelotti.

Mourinho na kikosi chake kinachosuasua cha Tottenham kilikaribisha Ancelotti na London leo Jumatatu kwenye mchezo wa Ligi Kuu England.

Bosi huyo wa Spurs, Mourinho amemsifia Ancelotti kuelekea kwenye mchezo huo na kwamba atavunja sheria ya kutosogelea kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, ili amkumbatie.

"Nafikiri kila mtu kwenye soka anavutiwa na Carlo (Ancelotti) kama kocha," amesema Mourinho akiwaambia waandishi wa habari.

"Kama humjui yeye kama tu basi mfahamu kama kocha. Nampenda yeye kama mtu na naweza kusema hivyo kwa kujisifu kabisa, kwani yeye ni mmoja wa makocha bora duniani.

"Nafikiri ni heshima Ligi Kuu England kuwa na mtu kama Carlo. Pia ni fahari kwa Everton kuwa na kocha kama yeye, unaweza kumwita vyovyote utakavyo."

Tottenham imeshinda mechi moja tu kati ya tisa zilizopita kwenye mashindano yote na walifungwa mabao 3-1 na Sheffield United Alhamisi.





# UNITED YAMPA PRESHA LAMPARD

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard amewataka wachezaji wake kuikumbatia presha ya kujaribu kufuzu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati wakipigania nafasi hiyo na Manchester United iliyorudi kwenye kiwango chake.

Lampard na Chelsea yake walirudi kwenye nafasi ya nne katika msimamo wa Ligi Kuu England baada ya kushinda magoli 3-0 dhidi ya Watford, huku United ikikaa kwenye nafasi hiyo kwa muda baada ya ushindi wa mabao 5-2 dhidi ya Bournemouth.

Chelsea wapo nafasi ya nne, wakiongoza kwa pointi mbili zaidi ya United, huku zikiwa zimesalia mechi tano kumalizika kwa ligi hiyo na hivyo wanapigania nafasi hiyo ili kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Na Lampard amewaambia wachezaji wake kutoifikiria United, ambayo imecheza mechi 16 bila kupoteza kwenye mashindano yote.

"Nafikiri kila mchezo utakuwa na presha sasa," amesema Lampard akiwaambia waandishi wa habari.

"West Ham ndio ilikuwa presha kubwa kwa sababu tulijua tungekwenda nafasi ya tatu. Ni presha tofauti, lakini lazima tuangalie kazi iliyopo mbele yetu."

# Flick amtabiria neema Lewandowski

**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA Mkuu wa Bayern Munich, Hansi Flick amesema, Robert Lewandowski anaweza kushinda tuzo ya Ballon d'Or baada ya kufikisha mabao 51 msimu huu na kutwaa ubingwa wa Ujerumani na DFB-Pokal.

Lewandowski alifunga mara mbili wakati Bayern wakipata ushindi wa mabao 4-2 dhidi ya Bayer Leverkusen Jumamosi kwenye fainali ya DFB-Pokal na kulitwaa taji hilo kwa mara ya pili mfululizo.

Baada ya David Alaba na Serge Gnabry kuiweka mbele Bayern, Lewandowski alifanya yake kipindi cha pili kwa kufunga mabao mawili dakika ya 59 na 89 kwenye mchezo huo uliopigwa mjini Berlin.

Huo ulikuwa mwendelezo wa kiwango bora zaidi cha Lewandowski kwa msimu huu 2019/20 baada ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland kuwa nyota kwa timu hiyo kwenye Ligi Kuu Ujerumani.

Lewandowski ndiye mfungaji bora wa Bundesliga akiwa na mabao 34 na aliiwezesha Bayern kushinda taji lake la tisa mfululizo, huku pia akiwa amefunga mabao 11 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Flick alisema Lewandowski anaweza kushinda tuzo ya Ballon d'Or msimu huu na aliwaambia waandishi wa habari: "Mabao 51 tayari yanamfanya kuwa imara.

"Naamini kuwa ana nafasi kubwa ya kubeba tuzo hii msimu huu, kwani kiwango chake kimeonekana na kuwa mtu mwenye nafasi nzuri zaidi."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO AWEKA REKODI JUVENTUS

**Ni mshambuliaji wa kwanza wa klabu hiyo kufikisha mabao 25 kwa msimu mmoja tangu...**

**TURIN,** Italia

BAO la frikiki lililofungwa na Cristiano Ronaldo limemweka Mreno huyo katika rekodi mpya akiwa na Juventus huku golikipa, Gianluigi Buffon naye akiweza rekodi ya kucheza mechi yake ya 648 ya Serie A kwa vinara wa ligi hiyo wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Torino hapo juzi.

**Ronaldo alifunga bao hilo dakika ya 55 na kumfanya aweke rekodi mpya ya kuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao zaidi ya 25 kwenye Ligi Kuu tatu tofauti, za England, Hispania na Italia.**

Buffon, ambaye ana umri wa miaka 42, amevunja rekodi iliyokuwa inashikiliwa na Paolo Maldini katika Serie A, baada ya kuchukuliwa tena kwenye ligi hiyo mwaka huu.

Paulo Dybala aliiweka Juventus mbele katika mchezo huo baada ya nyota huyo kutoka Argentina kuwatoka mabeki wawili na kufunga kwenye dakika ya tatu ya mchezo huo akimaliza pasi kutoka kwa Juan Cuadrado.

Nyota huyo kutoka Colombia alifunga bao la pili dakika ya 26, huku ikifunga bao pekee katika mchezo huo kwa penalti kupitia kwa Andrea Belotti dakika ya 45.

Ronaldo alifunga bao hilo lililomweka kwenye rekodi mpya dakika ya 61, kumfanya afikie rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza kufunga magoli 25 kwa msimu mmoja kwenye kikosi cha Juve tangu mwaka 1961.

Pia ni bao lake la kwanza la frikiki, katika frikiki 43 alizopiga ndani ya misimu miwili aliyoitumikia Juventus.

"Tumeendelea kuongoza vizuri na kufunga tena. Labda ni kwa sababu tulifikiria itakuwa kazi rahisi, lakini penalti waliyopata ilitufanya tupoteze umiliki wa mchezo," alisema Kocha wa Juventus, Maurizio Sarri.

Baada ya mechi, Ronaldo alisema: "Tulijua haitakuwa mechi rahisi, lakini tulistahili kupata ushindi, tulicheza vizuri.

"Goli langu? Nilikuwa nasubiri kufunga kwa frikiki. Nina furaha, lakini muhimu ni kushinda bila kujua ni nani wamefunga. Timu yetu inaendelea kuimarika, hilo ndio jambo muhimu."

Ushindi huo umeifanya Juventus kufikisha pointi 75 katika mechi 30 ilizocheza na kuendelea kukaa kileleni katika msimamo wa Serie A.

## ZISIKUPITE

### CHELSEA, HAVERTZ SAFI

CHELSEA imeamini kufanikiwa kwao kumsajili kiungo Mjerumani, Kai Havertz kutoka Bayer Leverkusen kumetokana na Mkurugenzi Mtendaji wa Bayern Munich, Karl-Heinz Rummenigge kusema klabu hiyo haina uwezo wa kumnasa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 katika majira ya joto. ***(Sun on Sunday)***

### PALMIERI ANUKIA INTER

INTER Milan imeanza mazungumzo na Chelsea kwa ajili ya kumnunua beki wa kushoto wa Timu ya Taifa ya Italia, Emerson Palmieri (25), kutoka kwa klabu hiyo ya Stamford Bridge. ***(Observer)***

### MADRID KUMTOA RODRIGUEZ

REAL Madrid inataka kumuuza kiungo mchezeshaji wake kutoka Colombia, James Rodriguez (28), ambaye amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake, ili kutosubiri kumruhusu aondoke akiwa mchezaji huru mwakani. Arsenal, Everton, Manchester United na Wolves zimeonyesha nia ya kumhitaji nyota huyo. ***(Marca)***

### MATA KUTUA FENERBAHCE

KIUNGO wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Hispania, Juan Mata, ambaye ana umri wa miaka 32, anataka kujiunga na Fenerbahce ya Uturuki ifikapo majira ya joto. ***(Sansursuz Futbol, via Sunday Express)***

### LACAZETTE KUUZWA

ARSENAL inajipanga kumuuza kiungo Mfaransa, Matteo Guendouzi (21), mshambuliaji, Alexandre Lacazette (29), au kiungo kutoka Uruguay, Lucas Torreira (24), ili kupata fedha za kumsajili kiungo wa Atletico Madrid na Timu ya Taifa ya Ghana, Thomas Partey (27). ***(Mail on Sunday)***

### VESTERGAARD SOKONI

LEICESTER City itajaribu kuwania tena saini ya beki wa Timu ya Taifa ya Denmark, Jannik Vestergaard kutoka Southampton, baada ya kumkosa katika dirisha dogo la usajili la Januari mwaka huu. ***(Goal)***

### MINA ANUKIA VALENCIA

VALENCIA inajiandaa kumsajili beki wa kati wa Everton na Timu ya Taifa ya Colombia, Yerry Mina, ambaye ana umri wa miaka 25. ***(Sun on Sunday)***

### SPURS YAMTAKA HOJBJERG

KIUNGO wa Southampton na Timu ya Taifa ya Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg, anawaniwa na Tottenham, ambayo pia imeweka wazi inataka saini ya beki wa kulia wa Norwich City, Max Aarons ambaye ana umri wa miaka 20. ***(Athletic, via Sunday Express)***

### SAINT-MAXIMIN KUTUA PSG

PARIS St-Germain imeonyesha nia ya kumsajili winga wa Newcastle United Mfaransa, Allan Saint-Maximin, ambaye ana umri wa miaka 23. ***(Mail on Sunday)***

### PALACE YAMTAKA GALLAGHER

MABOSI wa Crystal Palace wanajiandaa kupeleka ofa ya pauni milioni 10 ili kumnasa kiungo wa Chelsea, Conor Gallagher. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 20 amekuwa na msimu mzuri alipokuwa akiichezea kwa mkopo Charlton na Swansea. ***(Sun on Sunday)***

HABARI MICHEZO

## Mzizima, Arusha, Iringa zachuana

**Na Saada Akida**

CHAMA cha Mbio za Magari Tanzania (AAT), kimesema kimepokea maombi kutoka katika klabu tatu nchini zinazohitaji kuwa mwenyeji wa mashindano ya mwaka huu, imeelezwa.

Ofisa Uhusiano wa AAT, Athumani Hamisi, ameliambia gazeti hili klabu zilizoomba kuandaa michuano hiyo zinatoka katika mikoa ya Arusha, Iringa na Mzizima ya jijini, Dar es Salaam.

Hamisi alisema katika maombi yao, klabu hizo zimethibitisha zinauwezo wa kusimamia michuano hiyo kikamilifu.

Alisema waliamua kuanza maandalizi ya michuano hiyo baada ya kupata ruhusa ya kuendelea na mashindano kutoka katika Baraza la Michezo Tanzania (BMT).

"Morogoro wametujulisha hawawezi kuandaa mashindano ya mwaka huu kwa sababu wamekwama katika masuala la kifedha, tumewaelewa na tutashirikiana nao wakati mwingine wakiwa tayari," alisema Hamisi.

Aliongeza klabu ya Mount Usambara na Dar es Salaam hazijarudisha majibu kwa chama hicho juu ya kueleza na nafasi yao.

Alieleza ratiba ya mashindano hayo itatangazwa hivi karibuni baada ya kukamilika kwa sehemu ya mchakato wa maandalizi.

## ZFF yawasisitiza wadau kujipanga

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limewakumbusha waandishi wa habari za michezo kufuata taratibu zilizowekwa katika kipindi hiki cha hatua ya lala salama ya Ligi Kuu Zanzibar.

Kauli hiyo imetolewa baada ya baadhi ya waandishi kukaa muda mrefu wakisubiri kufunguliwa milango kushuhudia mchezo kati ya KMKM na JKU, uliochezwa juzi kwenye Uwanja wa Amaan.

Mkuu wa Ulinzi wa ZFF, Ramadhani Manyama, alisema waandishi hawazuiwi kuingia uwanjani kutekeleza majukumu yao, lakini wanatakiwa kufika mapema ili kuondoa usumbufu.

Manyama alisema wanakabiliwa na changamoto ya mashabiki kujitokeza na kusimama kwenye mageti wakati mechi zikiendelea hali ya kuwa serikali haijaruhusu mashabiki kuingia viwanjani.

"Tutakumbana na changamoto ya mashabiki kujazana kwenye mageti la kuingia uwanjani, hali hii inatupa usumbufu, tunashindwa kuwaingia mapema wahusika waliorodhesha kuingia uwanjani wakiwamo waandishi," alisema Manyama.

Aliwataka mashabiki na wadau wa soka kufuata maagizo yaliyotolewa na serikali kwa kufuatilia mechi za ligi hiyo kwa njia za redio na mitandao ya kijamii.

"Kwa kifupi ni suala la wahusika wote kufika kwa wakati, hatuzuii waandishi kuingia uwanjani, lakini lazima wafuate utaratibu ili kujiepusha na usumbufu, hii inawaweka kwenye wakati mgumu walinzi wetu," Manyama alisema.

# SIMBA QUEENS, JKT HATUMWI MTOTO LEO

**Na Saada Akida**

SAFARI ya kuwania taji la Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, inatarajia kuendelea tena leo kwa Simba Queens kuwakaribisha mabingwa watetezi wa ligi hiyo, JKT Queens katika mchezo utakaofanyika kwenye Uwanja wa Simba Mo Arena ulioko Bunju jijini, Dar es Salaam.

Vinara wa ligi hiyo, Simba Queens wenye pointi 35 watashuka dimbani wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 10-0 walioupata ugenini dhidi ya Ruvuma Queens, wakati JKT Queens yenye pointi 29 wao waliiadhibu Tanzanite Queens magoli 12-0.

Kocha Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', aliliambia gazeti hili wamejipanga kuendelea kutoa 'dozi' ili wafikie malengo ya kutwaa ubingwa wa ligi hiyo kwa mara ya kwanza msimu huu.

**Mgosi alisema anafahamu mechi hiyo itakuwa na ushindani, lakini wachezaji wake wamejiandaa kuonyesha ubora wao.**

"Sisi kila mechi kwetu ni sawa na fainali, tutaingia uwanjani kwa tahadhari ili tukicheza kwa umakini, hakuna mechi rahisi msimu huu, kila timu ina malengo yake," Mgosi alisema.

Nahodha wa Simba Queens, Mwanahamisi Omary 'Gaucho', alisema wachezaji wote wamejiandaa vizuri kuelekea mechi hiyo na wamejipanga kuondoka na pointi tatu muhimu.

Gaucho alisema wanataka kupata ushindi ili kuwafurahisha mashabiki wao kama walivyofanya 'kaka' zao kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo ni kati ya Alliance Girls dhidi ya Panama Girls wakati Baobab Queens watawakaribisha Marsh Queens huku Yanga Princess watawafuata Mlandizi Queens kwenye Uwanja wa Mabatini Mlandizi, mkoani Pwani.




Wachezaji wa Simba Queens wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania dhidi ya JKT Queens itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Simba Mo Arena ulioko Bunju jijini, Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA SC**

# KMKM yapunguzwa kasi Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MABAHARIA wa KMKM wamepunguzwa kasi baada ya kukubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa JKU katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mau A visiwani hapa juzi.

Bao pekee katika mchezo huo lilifungwa na Shehu Bulama, dakika ya 48.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa KMKM, Ame Msimu, alisema wachezaji wake walicheza vizuri, lakini hawakuwa na bahati ya kupata alama tatu katika mchezo huo.

Msimu alisema walikutana na timu ngumu na yenye uzoefu, lakini wanajipanga kufanya vema katika mechi zinazofuata ili watimize malengo waliyonayo.

"Wachezaji wetu walicheza vizuri, lakini mchezo ulikuwa mgumu sana pia walikosa umakini katika kuzitumia vema nafasi walizozipata, na kosa moja walilofanya lilisababisha wapinzani wetu kulitumia kosa hilo hatimaye wakatufunga," alisema Msimu.

Aliongeza wanaamini watafanya vema katika mechi yao dhidi ya Mlandege itakayochezwa Julai 13, mwaka huu.

Katika mechi nyingine ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Gombani juzi, Chipukizi walilazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Machomane United.

Sare hiyo imeifanya Chipukizi kuendelea kuburuza mkia katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16.

Ligi hiyo itaendelea leo kwa Jamhuri kuikaribisha Zimamoto kwenye Uwanja wa Gombani wakati Chipukizi itawavaa Mafunzo na Kipanga itacheza dhidi ya Jang'ombe Boys.

# Michezo

Jumatatu Julai 6, 2020

Nipashe




Ronaldo aweka rekodi Juventus UKURASA 22



Beki wa kati wa Arsenal, David Luiz (kushoto), akipambana kuwania mpira dhidi ya straika wa Wolves, Adama Traore katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa kwenye Uwanja wa Molineux juzi usiku. Arsenal ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# Simba, Yanga zabanwa

## Mchuano mkali waendelea katika vita ya kujinasua na janga la kushuka daraja...

**Na Adam Fungamwango**

VIGOGO wa soka nchini, Simba na Yanga zilishindwa kufurukuta ugenini baada kulazimishwa suluhu na timu za Ndanda FC ya Mtwara na Biashara United ya Mara, katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara zilizochezwa jana.

**Mabingwa wa msimu huu, Simba, wakiwa kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona waliondoka na pointi hiyo moja huku wenyeji Ndanda walioko katika hatari ya kushuka daraja wakionyesha kandanda safi.**

Kwenye mechi hiyo, Simba ilionekana kucheza mchezo wa taratibu na pasi nyingi, huku Ndanda ikionekana inatafuta ushindi au japo sare ili kujiongozea hazina ya pointi kwa ajili ya kujiondoa kwenye janga la kushuka daraja.

Ilikuwa ni sare ya pili mfululizo kwa Wekundu wa Msimbazi, baada ya Jumapili ya Juni 28, mwaka huu kutoka sare ya bila kufungana dhidi ya Tanzania Prisons kwenye Uwanja wa CCM, Sokoine jijini, Mbeya.

Dakika ya 29, Luis Miquissone wa Simba alipiga shuti la kustukiza, lakini lilitemwa na kipa, Ally Mustapha 'Barthez', kabla ya kuokolewa na mabeki wa Ndanda huku nahodha wa mabingwa hao, John Bocco alikaribia kuipatia timu yake bao dakika ya 38, baada ya kuunganisha kwa kichwa krosi iliyopigwa na Deo Kanda, lakini mpira ulitoka kidogo nje ya lango la Ndanda.

Simba ilikosa tena bao la wazi dakika moja kabla ya kwenda mapumziko, baada ya Kanda kupiga 'tik-tak', akiunganisha krosi ya Miquissone, lakini mpira ukatoka tena nje ya lango. Miquissone ambaye kwenye mechi ya jana ndiye alikuwa kivutio kwa kucheza kandanda safi, nusura tena aifungie Simba bao dakika ya 71, alipopiga shuti lililowababatiza mabeki wa Ndanda na kurejea uwanjani.

Aishi Manula aliiokoa Simba kufungwa bao dakika ya 74 kutokana na shuti la juu lililokatika kama upinde wa mvua, lakini Manula aliruka juu kwa ustadi na kudokoa mpira ukatoka sentimeta chache juu ya lango la Simba na kuwa kona ambayo haikuwa na madhara. Kwa matokeo hayo, Simba imefikisha pointi 80 na kuendelea kukaa kileleni wakati Ndanda wamefikisha pointi 36 na kupanda hadi nafasi ya 17.

Kwenye Uwanja wa Karume, Musoma Yanga ilijiongezea pointi moja na kufikisha pointi 61, baada ya kulazimishwa sare ya bila kufungana na wenyeji Biashara United ambayo ina rekodi nzuri ikiwa nyumbani msimu huu.

Timu zote zilicheza mchezo wa kukamiana, nguvu na mipira mirefu, kiasi cha kufanana kwa kila kitu.

Ditram Nchimbi alipiga mpira ovyo, dakika ya 47, akiwa kwenye nafasi nzuri ya kufunga bao, baada ya mabeki wa Biashara United kujichanganya wakati dakika ya 55, wachezaji watatu wa Yanga, Lamine Moro, Nchimbi, na David Molinga, waliingia wenyewe nyavuni, wakiwa kwenye harakati za kutaka kuunganisha mpira wa faulo uliopigwa na Juma Abdul.

Dakika saba kabla ya pambano hilo limalizika, nusura Yanga iandike bao, baada ya Juma Makapu kupiga kichwa mpira wa kona uliopigwa na Patrick Sibomana, lakini ukapaa juu ya lango.

Yanga ilikuwa kwenye nafasi ya pili, kabla ya mechi ya jana usiku kati ya Azam FC dhidi ya Singida United, huku Biashara United ikiwa kwenye nafasi ya tisa kwa pointi 45.

Kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza, Alliance FC ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Mtibwa Sugar na matokeo hayo, yanawafanya wakazi wa Manungu, Turiani mkoani Morogoro kufikisha pointi 38, wakati Alliance wao wana pointi 37, lakini timu zote zikitakiwa kupambana kujinasua na hatari ya kushuka daraja.

# Simba yainyima 'usingizi' Namungo

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Mrundi, Thiery Hitimana, amesema ana 'kazi kubwa' kuhakikisha nyota wa Simba hawafurukuti katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaowakutanisha keshokutwa kwenye Uwanja wa Majaliwa, mkoani Lindi.

Namungo FC itakuwa wenyeji wa mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba katika mchezo wa raundi ya 33 na baada ya mechi hiyo, Wekundu wa Msimbazi watakabidhiwa kombe lao la ubingwa.

Hitimana aliliambia gazeti hili ana 'kibarua kinene' kuhakikisha anapanga kikosi imara ili kukabiliana na wachezaji wa Simba, ambao wanauzoefu na wana kiu ya kuendelea kushinda.

Kocha huyo alisema aliiangalia vema mechi kati ya Simba na Azam, na ameahidi kuwakabili nyota wapinzani wao kwa namna mpya.

"Niliuangalia mchezo wa robo fainali ya FA, Simba na Azam, kwa kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wa kikosi cha Simba, ninaamini nitakuwa na mechi ngumu, nimecheza na Simba mzungumzo wa kwanza, sikuwa na presha kama ilivyokuwa sasa, ukisema umkabe Chama (Clatous), basi kuna yule wa Msumbiji (Luis Miquissone) ni hatari, Kagere (Meddie), ninamfahamu, hana mchezo," Hitimana alisema.

Aliongeza amewataka wachezaji wake kutulia na kufuata maelekezo, kwa sababu mpira ni mchezo wa makosa na endapo wapinzani wao watateleza, watatumia vema nafasi hiyo.

"Nakiandaa kukabiliana na mchezaji yoyote, siwezi kutoa maelekezo ya kumzuia Chama au Kahata (Francis), wakati anakuja kucheza Deo Kanda au Miraji Athuman," aliongeza kocha huyo.

Hitimana alisema mbali na Simba kuwa vizuri pia kitendo cha kukabidhiwa kombe mbele yao kinawapa wakati mgumu katika kusaka ushindi kwenye mchezo huo.

"Suala la kukabidhiwa kombe kwetu wametupa mtihani mkubwa, kwa sababu hawatahitaji kuona wanapokea kombe tena baada ya kufungwa," Hitimana aliongeza.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042